

GRAFOLOJIA KATIKA UCHAPAJI WA RIWAYA YA *MKAMANDUME*

TASNIFU

YA

ELIUD TEYIE MUSOTSI

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA IDARA YA KISWAHILI KATIKA CHUO
KIKUU CHA KENYATTA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI**

2017

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa chuoni humu wala katika chuo kingine kwa madhumuni ya shahada yoyote.

Sahihi..... Tarehe.....

ELIUD TEYIE MUSOTSI

NAMBARI YA USAJILI: C50/24713/2011

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioidhinishwa na chuo kikuu cha Kenyatta.

Sahihi..... Tarehe.....

DKT. JOSEPH NYEHITA MAITARIA

Mwenyekiti, Idara ya Lugha

Chuo Kikuu cha Karatina

Sahihi..... Tarehe.....

DKT. RICHARD MAKHANU WAFULA

Idara ya ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwa na kibali cha kuelimika. Kwa wazazi wangu wapendwa Bw. Epaenitus Inzofu na Bi. Mary Inzofu, ndugu zangu Carey Francis, Dorine Namwendwa, Robert Wabuko, Vincent Khwale na wanangu Kevin na Michelle Amusugut Teyie, ahsanteni kwa kunivumilia.

SHUKRANI

Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, nguvu afya njema na uwezo wa kuikamilisha kazi hii. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Joseph Maitaria, ambaye kwa sasa ni mwenyekiti wa idara ya Lugha, chuo kikuu cha Karatina na Dkt. Richard M. Wafula, ambaye kwa sasa ndiye mwenyekiti wa idara ya Kiswahili, chuo kikuu cha Kenyatta. Mlinielekeza vyema na kwa wakati, Mungu awe nanyi na aendelee kuwanehemesha.

Shukrani zangu pia ziwafikie wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili, chuo kikuu cha Kenyatta kwa kunifundisha vyema katika masomo ya kiwango cha uzamili, nao ni Prof. Mbaabu, Prof. King'ei, Prof. Ndung'o, Dkt. Arege, Dkt. Masinde, Dkt. Osore, Dkt. Onyango, Dkt. Ngugi, Dkt. Gakuo, Dkt. Mwhaki, Bi. Mudhune, Bi. Gathenji, Bw. Mugambi, Bw. Kamunde na Bw. Mukobwa.

Shukrani zingine ziwafikie wote walioshirikiana nami kwa njia mbalimbali kufaulisha masomo haya wakiwemo Meja mtaafu Peter Murunga, mkewe Rose Murunga na wanao wote, bila kumsahau Noel Lutomia aliyenifaa sana wakati wa maandalizi ya utetezi wa mada ya utafiti huu. Siwezi kuwasahau wazee Bennie Orwako na Jenerali Mstaafu Hezron Murunga kwa kunienzi kwa vyovyote mlivyofanya. Mwisho kabisa, ningependa kuwashukuru Ntawiyinga, Mwilaria, Everlin Onyango, Brendah Egara, Omuya, Nanjala, Oginda, Wamboi na Pamela Onyango ambao tulisoma nao wakati huo chuoni. Ushirikiano wenu ulinitia moyo katika safari hii.

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza mchango wa vipengele vya kigrafolojia katika uchapaji wa riwaya ya *Mkamandume* ya Said A. Mohamed. Uliviangazia vipengele hivyo kwa kutathmini jinsi vilivyotumika na athari kwa msomaji wa riwaya teule na utanzu wa riwaya kwa jumla. Utafiti uliongozwa na nadharia ya kimtindo iliyoasisiwa na Baally (1909) na kuenezwa na Jakobson (1958) na Halliday (1971) na kisha kuelezewa na akina Leech na Short (1981). Aidha, mitazamo ya Leech na Short (1981) ilizingatiwa zaidi. Kulingana nao, mojawapo ya dhana ya kimtindo inahusu matumizi ya vipengele vya kigrafolojia kama vile viakifishi, herufi kubwa, tahajia, *mlazo* na hata kugawika kwa maandishi kwa aya kadha miongoni mwa vipengele vingine vya kiisimu. Kiupeo, utafiti huu ulijikita katika riwaya ya *Mkamandume*, na ulishughulikia vipengele hivyo vya kigrafolojia riwayani. Utafiti ulifanyiwa maktabani ambamo nilisoma kwa kina vitabu mbalimbali kuhusu mada na nadharia ya kimtindo. Data iliyokusanywa, ilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti pamoja na msingi wa nadharia ya kimtindo. Data hiyo iliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Ripoti ya utafiti ilipangwa katika sura tano. Sura ya kwanza ilijumulisha utangulizi ambamo usuli wa mada ya utafiti, suala, maswali ya utafiti, malengo, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa nadharia, pamoja na mbinu za utafiti zilirejelewa. Sura ya pili ilianguzia riwaya ya kisasa katika miktadha ya Kimagharibi na Uswahilini. Sura ya tatu iliihakiki riwaya ya *Mkamandume* huku vipengele vya kigrafolojia; viakifishi vilivyotumika na mwandishi vikijadiliwa. Katika sura ya nne tulijadili vipengele vingine vya kigrafolojia visivyokuwa viakifishi ambavyo mwandishi alivitumia katika ujenzi wa riwaya huku athari yavyo ikichanganuliwa. Sura ya tano ilijumulisha ufupisho wa yaliyotangulia. Utafiti huu ulilenga kuwanufaisha wanafunzi, wasomaji, wahakiki na wandishi wa riwaya kwa ujumla.

ABSTRACT

The study investigated the role of graphological features used in the Kiswahili novel *Mkamandume* authored by Said A. Mohamed. It looked at various graphological features used in the novel and their impact on the reader. The research was guided by the theory of stylistics pioneered by Baally (1909) and propagated by Jakobson (1958), Halliday (1971) and expounded by Leech and Short (1981). More emphasis was however placed on the views of Leech and Short (1981). According to these theorists, the concept of stylistics also entails the use of graphological features such as capitalization of words, use of italics, bold, paragraphing, punctuations among other linguistic features. In terms of delimitations of the study, this research was basically concerned about graphological features used in the selected novel and how they impact on the reader. This descriptive research was conducted in the library where I had the opportunity to access and read more literature about the topic of research as well as the theory of stylistics. Data collected was sorted out and analysed on the basis of the research objectives and in conformity with the principles of the guiding theory. Data presentation was done through written explanations. This research was presented in five chapters where chapter one comprised of the introduction which covered the background, research problem, research questions, research objectives, significance of the study, scope, literature review, theoretical framework as well as the research design. Chapter two looked at the modern novel in the context of western literature as well as Swahili literature. Chapter three was a summary of the novel *Mkamandume* and an analysis of how punctuations have been used by the writer in the build-up of the novel. Chapter four was an analysis of other graphological features used by the author other than punctuations to accomplish his work and their impact on the reader. Chapter five was a summary of all that was researched. The research outcome was expected to benefit students, scholars, researchers as well as authors of novels.

UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU

Grafolojia : Tawi la isimu linalochunguza uandishi na upigaji chapa kama mfumo wa ishara kwa kutumia teknolojia yoyote; kalamu, kichapishi, shirika la uchapishaji au skrini ya kielektroniki.

Mtindo: Namna ya kujieleza kwa kutumia lugha au jinsi mwandishi wa kazi ya sanaa anavyowasilisha ujumbe wake.

Uchapaji: Matumizi ya vipengele vya kigrafolojia katika kazi yoyote ya utunzi.

Uchimuzi: Matumizi ya mbinu za kimuundo ambazo zinakiuka uandishi wa kawaida kwa lengo la kukifanya kipengele fulani kionekane zaidi ya vingine.

YALIYOMO

MADA

IKIRARI	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI.....	iv
ABSTRACT.....	vi
UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU.....	vii
YALIYOMO.....	viii
SURA YA KWANZA	1
1 Utangulizi	1
1.1. Usuli wa mada.....	1
1.2. Suala la utafiti	6
1.3 Maswali ya Utafiti.....	8
1.4 Malengo ya utafiti	8
1.5 Sababu za kuchagua mada	9
1.6 Upeo na mipaka.....	10

1.7	Yaliyoandikwa kuhusu mada	11
1.7.1	Dhana ya grafolojia na fasihi	11
1.8	Misingi ya Nadharia	15
1.8.1	Dhana ya Mtindo na Kimtindo	18
1.8.2	Mihimili muhimu ya nadharia ya kimtindo.....	29
1.9	Mbinu za utafiti	30
1.9.1	Muundo wa utafiti.....	30
1.9.2	<i>Mahali pa utafiti</i>	30
1.9.3	Sampuli lengwa	31
1.9.4	Mbinu za ukusanyaji wa data	31
1.9.5	Uchanganuzi wa data	32
1.9.6	Uwasilishaji wa Matokeo	32
1.9.7	Kiishilio	32
SURA YA PILI: RIWAYA YA KISASA.....		33
2.	Utangulizi	33
2.1	Dhana ya riwaya ya kisasa.....	33

2.2 Msingi wa riwaya ya Kiswahili	39
2.3 <i>Dhana ya riwaya ya Kiswahili ya kisasa.</i>	44
2.4 <i>Kiishilio</i>	48
SURA YA TATU: RIWAYA YA MKAMANDUME	49
3 Utangulizi	49
3.1 Hatua za usomaji mwema	49
3.2 Uchanganuzi wa matini (<i>Riwaya ya Mkamandume</i>).....	54
3.3 <i>Viakifishi na jinsi vilivyotumika katika ujenzi wa riwaya ya Mkamandume.</i>	60
3.3.1 Viakifishi vya neno	61
3.3.1.1 Ving'ongo (')	61
3.3.1.3 Alama za kunukuu (‘ ’) (“ ”)	65
3.3.1.4 Vinyota (***)	66
3.3.2 Viakifishi vya ndani.....	67
3.3.2.1 Kituo, Koma au Kipumuo (,)	67
3.3.2.2 <i>Koloni</i> (:):.....	71
3.3.2.3 <i>Semi koloni</i> (;):.....	72

3.3.2.4 Mabano ().....	74
3.3.2.5 Deshi (—).....	75
3.3.2.6 Udondoshaji (...)	75
3.3.3 Viakifishi tamati au vya nje.....	76
3.3.3.1 Kikomo (.).....	77
3.3.3.2 Kiulizi (?).....	78
3.3.3.3 Alama ya kihisishi (!)	79
3.4 Viakifishi kimuundo	80
3.5 Kiishilio	82
SURA YA NNE.....	84
VIPENGELE VINGINE VYA KIGRAFOLOJIA VISIVYOKUWA VIAKIFISHI	84
4 Utangulizi	84
4.1 Maandishi ya mlazo	84
4.2 Herufi kubwa	87
4.3 Herufi nzito	87
4.4 Fonti za maneno	88

4. 5 Kiishilio	89
SURA YA TANO	90
UFUPISHO WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO PAMOJA NA.....	90
MAPENDEKEZO.....	90
5. Utangulizi	90
5.1 Muhtasari wa utafiti.....	90
5.2 Matokeo ya utafiti	92
5.3 Changamoto katika utafiti.....	93
5.4 Mapendekezo kwa ajili za tafiti za baadaye	94
MAREJELEO.....	95

SURA YA KWANZA

1 Utangulizi

1.1. Usuli wa mada

Jukumu la sanaa kwa kawaida ni kumwezesha binadamu kuufahamu ulimwengu kwa njia tofauti na kwa kufanya hivyo, sanaa wakati mwingine huchepuka kutoka kwa ukawaida wake. Sanaa ya fasihi andishi imedhihirisha wazi kuwa kuna uhusiano wa ufaano kati ya isimu na fasihi, ambao unastahili kuchukuliwa kama uhusiano wa ufasiri na mwanga wa maafikiano. Waandishi wengi wa fasihi huibuka na njia mbalimbali za kuendeleza kazi zao, miongoni mwa njia hizo ni matumizi ya vipengele vingine vya kiisimu visivyo maneno.

Wanapoandika kwa njia hii, huwa hawalengi kuendeleza maono na ujumbe wao kisanaa tuu bali pia kuyaafikia maazimio yao pamoja na kutimiza matukio kwa utaratibu usiozoeleka. Kwa kufanya hivyo, waandishi huwa wanaijenga na kuiendeleza mitindo yao kipekee. Kando na hilo utaratibu huo pia huleta upatanisho kati ya dhana mbalimbali ikiwa ni pamoja na isimu na fasihi.

Ni dhahiri kuwa katika uandishi wa riwaya, dhana ya uchapaji huendelezwa na kurejelewa ambayo ni muhimu katika kufaulisha mawasiliano. Watalaam akiwemo Ogunsiji (2007) wanasema kuwa kando na matumizi ya maneno katika ujenzi wa utanzu wa riwaya, mwandishi anaweza kutumia alama zingine zisizo maneno katika kuiendeleza kazi yake, na

kwamba alama hizi zisipuuzwe kwa vile huwa zimebeba ujumbe fulani. Miongoni mwa alama hizo ambazo Ogunsiji (keshatajwa) ameshughulikia ni viakifishi, tahajia, rangi, michoro na vipengele vingine vingi ambavyo amesema hubeba ujumbe mwingine tofauti na maneno katika makala, na hivyo basi huwa na athari fulani kwa msomaji wa kazi hiyo.

Kwa mujibu wa Ogunsiji (keshatajwa), alama hizi hujulikana kama alama za kigrafolojia. Dámová (2007) katika uainisho wake wa viwango mbalimbali ambavyo wanamitindo huvitumia katika uhakiki wa matini, anataja grafolojia. Anasema kuwa grafolojia ni kiwango katika uhakiki wa lugha ambacho huchunguza mifumo ya uandishi na kaida za uendelezaji wa maneno.

Marie (2013) anasema kuwa kuna uwezekano wa mwaandishi wa sanaa kutumia michoro katika kazi yake, na kwamba ikiwa atafanya hivyo, basi michoro hiyo itamwathiri msomaji wa kazi hiyo katika upokezi wake. Mawazo ya Ogunsiji yanashadidiana na ya Adegaju (2008), anayeongezea kwa kusema kuwa utaratibu wa mpangilio wa matini, matumizi ya aya pamoja na uchaguzi wa fonti ambazo mwandishi hutumia huathiri upokezi wa msomaji wa kazi hiyo.

Leech na Short (1981) wanasema kuwa matumizi ya vipengele hivyo vya kigrafolojia katika riwaya huwa na athari ya uchimuzi. Wanafafanua uchimuzi kama dhana yenye maana ya matumizi ya mbinu za kimuundo zinazokiuka uandishi wa kawaida kwa lengo la kukifanya kipengele fulani kionekana zaidi ya kingine.

Kulingana na Wamitila (2008), vipengele vya kigrafolojia vimeshughulikiwa kwa undani katika utanzu wa ushairi na wataalam mbalimbali na vimebainika kuwa na mchango mkubwa, ilihali utafiti wa kutosha haujafanywa kuhusu mchango wa vipengele hivyo vya kiisimu katika utanzu wa riwaya, hususan ya kisasa. Ni kutokana na pengo hilo ndiposa utafiti huu ulifanywa.

Kwa mujibu wa Wamitila (keshatajwa), miongoni mwa vipengele vya kigrafolojia ambavyo hutumika katika ujenzi wa riwaya za kisasa ni pamoja na viakifishi, herufi kubwa, topografia, urefu wa matini, fonti, herufi nzito, muundo wa aya miongoni mwa vingine. Utafiti huu ulichunguza matumizi ya vipengele hivyo vya kigrafolojia katika ujenzi wa riwaya ya kisasa na jinsi vinavyomuathiri msomaji.

Yoshifumi (1997) anasema kuwa uchapaji ni dhana muhimu katika uandishi na hujihusisha na upigaji chapa kwa kuangalia vipengele vingi ambavyo ni pamoja na matumizi ya herufi za mlazo, herufi kubwa, kistariungio, tahajia ya maneno, matumizi ya nafasi, kutia pengo katika maandishi pamoja na vipengele vingine vya kiisimu ambavyo huibua maana tofauti kwa msomaji vinapotumika katika utanzu wa riwaya. Anaendelea kutueleza kuwa ni dhana muhimu ambayo pia imebeba historia na fasihi ya binadamu au utamaduni wa binadamu kwa ujumla, kwa vile ilianza tu binadamu alipovumbua uwezo wa kuandika.

Kulingana na Yoshifumi (keshatajwa), uchapaji hivi leo ni taaluma muhimu yenye historia ndefu tangu mwasisi Camillo Baidi aishughulikia takribani karne tano zilizopita. Abb Jean Hippolyte aliiwekea taaluma hii kanuni mwafaka mwaka wa 1897 na kuiwezesha kufanyiwa utafiti wa kisayansi wa kwanza wakati huo. Mikakati ya mwasisi na waitifaki wa taaluma hii hivi leo umemwezesha binadamu kuchapisha matini kwa njia za kisasa, zikiwemo matumizi ya skrini za kielektroniki na hivyo basi kuibuka na mitindo mbalimbali ya uandishi miongoni mwa wandishi.

Kiiru (2003) anasema kwamba kuna waandishi mbalimbali na kwamba mwandishi wa kutajika ni yule mwenye uwezo wa kuibuka na uandishi mpya. Kulingana naye, hii hufanyika tu ikiwa mwandishi huyo atakiuka ukawaida wa uandishi kwa kuzivunja kaida za uandishi zilizoko ili achangeie katika uandishi unaodhihirirsha kuzuka kwa lugha mpya. Anasema kuwa huyu ni mwandishi ambaye kwa hakika atakuwa amekumbana na lugha ikijikokota na akailazimisha kutembea wima.

Yeibo (2014) anataja sifa bainifu za mwandishi bora kwa kusema kuwa ni yule mwenye uwezo wa kujitokeza na kutambulika miongoni mwa wenzake, huku upekee wake kimtindo ukidhihirika wazi. Hii ni kusema kwamba kuna uhusiano wa utegemeanobaina kati ya mfumo wa lugha na dhima ya lugha, uhusiano ambao hutumika na waandishi wa sanaa kujenga maumbo mbalimbali ya lugha inayowasilisha ujumbe na maono yao katika matini ya kifasihi, tofauti na matumizi hayo kiisimu.

Yeibo (keshatajwa) anasema kuwa hii inawezekana kutokana na kufulikana kwa lugha kama chombo cha mawasiliano ambacho chaweza kupata maumbo kadha kutokana na matukio ya kijamii. Kuifinyanga lugha kwa njia hii kimatini huibua dhana ya uchimuzi kifasihi. Longacre (1992) anasema kuwa uchimuzi ni dhana ambayo imefanyiwa utafiti mpana miongoni mwa lugha mbalimbali za Kiulimwengu zikiwemo Kiindonesia na hata Kifaransa cha Kirasimi. Kulingana naye, dhana hii ilitokana na wanamiundo wa shule ya kiisimu ya Praque, na ikaweza kupenyeza katika fasihi tambuzi ya kiakili.

Kwa mujibu Longacre (keshatjwa), dhana hii iliasisiwa na mwananadharia wa nchi ya Zeshoslovakia Jan Mukavrovsky aliyeshughulikia viwango mbalimbali vya mitindo katika fasihi. Anataeleza kuwa uchimuzi huweza kujitokeza katika matumizi ya lugha kimazungumzo kupitia kwa mhadhara, na pia kwa mandishi kupitia kwa majarida kinathari, lakini kujitokeza huku huwa bila utaratibu maalum. Anasema kuwa uchimuzi huwa na athari ya kufanya matini isionekane ya kawaida na hivyo basi kuathiri upokezi wa msomaji kisaikolojia.

Wakichangia, Miall na Kuiken (1995) wanaelezea uchimuzi kama mageuko tofauti ya kintindo kimandishi, ambayo huleta hisia ya kuzidisha muda wa kusoma matini. Wanasema kuwa kwa kufanya hivyo, uchimuzi hunasa makini ya msomaji pamoja na hisia zake katika matini. Wanataeleza kuwa uchimuzi huwa na maumbo fulani ambayo hujitokeza hatua kwa hatua, na pia huwa na uhusiano wa kimsonge.

Kwa mujibu wa mtazamo wa Miall na Kuiken (weshatajwa), hii ina maana kuwa vitu vyenye mfanano huweza kujirejelea, na kiolezo hiki cha mshabaha huenda kikavitawala vingine. Kulingana nao, uchimuzi katika fasihi hutumika ili kufanya vitu visijulikane waziwazi; kuvifanya vionekane tofauti miongoni mwa vingine au kuzidisha urefu wa utambuzi, hii hufanyika kwa vile thibitisho la utambuzi ni tukio la kiujumi ambalo ni lazima lirefushwe.

Watafiti hawa tuliyowataja awali wanasema kuwa mojawapo ya vipengele vinavyotumika hivi leo kuchimuza kazi ya fasihi ni grafolojia. Kwa mujibu wa Crystal (1995), grafolojia ni tawi la isimu linalochunguza mfumo ya ishara inayotumika kuwasilisha lugha kwa njia ya kimaandishi. Anaendelea kutufahamisha kuwa mfumo huo wa kimaandishi hujumlisha othografia, stenografia, teknografia na pedografia.

Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa riwaya ya kisasa, ambayo mtindo wake wa kisimulizi ulionyesha ubunifu mkubwa kama vile maingiliano baina ya sauti ya kisimulizi na mhusika, mvunjiko wa mkondo na usimulizi pamoja na uchangamano wa kimuundo. Ni utafiti ambao ulitathmini mchango wa vipengele vya kigrafolojia na athari yavyo kwa msomaji wa riwaya teule na tanzu za riwaya kwa ujumla.

1.2. Suala la utafiti

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), uandishi wa fasihi kwa lugha ya Kiswahili una mashiko makubwa katika ulimwengu wa leo. Hata hivyo, Mulokozi (keshatajwa) anasema kuwa uwasilishaji wa kazi za kifasihi kama vile riwaya hutegemea kwa kiasi kikubwa mwingiliano

baina ya fani na maudhui, licha ya kuwa upokezi wa kazi hiyo huathiriwa na vipengele vingi, vingine visivyo vya kifasihi hivi kwamba uhakiki kamili wa kazi hiyo ni vyema uvirejeele vipengele vyote, ili kutathmini jinsi vinavyohusiana na kuathiriana katika utendakazi.

Wataalam, akiwemo Wamitila (2008) na Chukwu (2010) wamebainisha kuwa upo uhusiano wa karibu sana kintindo kati ya usimulizi unaopatikana katika kazi fulani za kifasihi na uakifishaji.

Wamitila na Chukwu (weshatajwa) wanasema kuwa ingawa ni jambo la kawaida kwa kazi yoyote iliyoandikwa kuzingatia uakifishaji mwafaka, kuna vilevile uakifishi mitindo ya kisimulizi ya kazi za fasihi hasa za riwaya za kisasa, hivyo basi ipo haja ya kuliangalia suala zima la uakifishaji kwa jicho pekuzi. Hii ni kwa sababu kumezuka mitindo mipya ya uakifishaji katika riwaya, kinyume na matumizi ya viakifishi hivi katika taaluma ya isimu na katika utanzu wa ushairi, jambo linaloibua hamu na haja ya kufanyiwa utafiti. Viakifishi kwa sasa ni baadhi ya alama zinazotawala utanzu wa riwaya miongoni mwa vipengele vingine vya kigrafolojia kama vile vinyota, alama za mlazo, herufi kubwa, herufi nzito, fonti mbalimbali, katuni na hata michoro.

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa vipengele vya kigrafolojia katika ujenzi wa utanzu wa riwaya ya kisasa ya *Mkamandume*. Ulinuia kubainisha vipengele vya kigrafolojia vilivyotumika na athari inayoibuka kufuatia matumizi hayo.

1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo ;

- a. Je, grafolojia ni dhana muhimu katika ujenzi wa utanzu wa riwaya ?
- b. Ni vipengele vipi vya kigrafolojia ambavyo vimetumika katika ujenzi wa riwaya ya *Mkamandume* ?
- c. Vipengele hivi vina athari yoyote kwa msomaji wa riwaya ?

1.4 Malengo ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo ;

- i.) Kubainisha ikiwa vipengele vya kigrafolojia vilichangia katika ujenzi wa utanzu wa riwaya teule.
- ii.) Kutambua aina ya vipengele vya kigrafolojia vilivyotumika katika ujenzi wa utanzu wa riwaya ya *Mkamandume*.
- iii.) Kutathmini athari ya vipengele hivyo kwa msomaji wa riwaya teule y *Mkamandume* na utanzu wa riwaya kwa ujumla.

1.5 Sababu za kuchagua mada

Tahakiki nyingi za kifasihi za Kiswahili hazijaangazia suala la grafolojia na uchimuzi kintindo katika ujenzi wa utanzu wa riwaya kama ilivyo katika utanzu wa ushairi katika lugha ya Kiswahili. Kaluta (1954) anasema kuwa katika ujenzi wa utanzu wa ushairi, mshairi anao uhuru wa kupunguza silabi kwa mfano neno vile vile liwe vivile ilihali ni nini liwe n'ni. Pia mshairi anao uhuru wa kuzidisha mizani na kuibuka na maneno kama vile nenda badala ya enenda, sikia iwe sikiliza na aindeleze kazi yake bila ugumu wowote. Kando na uhuru huu, mshairi anao uhuru wa kuboronga sarufi na hata kutumia maneno ya kizamani. Kwa hivyo inabainika kuwa huu ni utaratibu uliokubalika katika ujenzi wa utanzu wa ushairi katika Kiswahili, tofauti na ilivyo katika ujenzi wa riwaya ya Kiswahili. Utafiti huu kwa hivyo ulichochea na nia ya kutathimini ikiwa matumizi ya vipengele vya kigrafolojia huchangia katika ujenzi wa utanzu wa riwaya, kama ifanyavyo katika utanzu wa ushairi, na athari zake kwa msomaji. Ni kutokana na mtazamo huu ndiposa mtafiti aliamua kuichagua mada hii.

Riwaya teule ya *Mkamandume* iliteuliwa kimaksudi kama mfano bora wa riwaya ya kisasa kwa sababu kutokana na usomaji wa kipailoti, mtafiti alibainisha kwamba inavyo vipengele kochokocho vya kigrafolojia. Aidha,riwaya ya mwandishi huyu ilichaguliwa kutokana na tajriba pana ya mwandishi huyu ya kuandika kazi zinazorejelea vipera vyote vya kazi za fasihi andishi ya Kiswahili kutoka kwa riwaya, hadithi fupi, mashairi na hata tamthilia.

Dhana ya grafolojia ilichaguliwa na mtafiti kufuatia usomaji mpana na kwamba, kwa sasa kumezuka mawasiliano yanayoendelezwa kwa matumizi ya ishara zisizo rasmi pasipo na maneno. Kwa mfano katika magazeti, tunakumbana na michoro ya vibonzo au katuni bila maneno. Ukizuru voo vya umma katika miji mingi nchini, utatambua kwamba kunazo ishara katika kuta za voo hivyo ambazo huwasilisha ujumbe fulani, hususan tunapokaribia uchaguzi wa kitaifa. Ufasiri wa ujumbe unaolengwa na njia hii ya mawasiliano hutegemea ujuzi aliyo nao msomaji.

Kwa hivyo dhana ya grafolojia ni eneo pana ambalo laweza kutafitiwa kwa taaluma mbalimbali, lakini mtafiti alionelea kuwa ilikuwa vyema ikiwa angeshughulikia dhana hii katika utanzu wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa.

1.6 Upeo na mipaka

Upeo wa utafiti huu ulijikita kwenye fasihi andishi hasa riwaya ya kisasa ya *Mkamandume*, ambapo niliangazia vipengele vya kigrafolojia ambavyo vilitumika *katika* ujenzi wa riwaya teule. Aidha ilitambulika kuwa vipengele hivi ni vingi na mtafiti alijikita katika viakifishi na mchango wake katika kuimarisha uchimuzi.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

1.7.1 Dhana ya grafolojia na fasihi

Leech na Short (weshatajwa) wameshughulikia dhana ya grafolojia kwa undani. Wametambua kwamba kwa kuwa riwaya huhifadhiwa kimaandishi, ni muhimu kujumulisha kipengele kingine katika mfumo wa uhakiki wa kimtindo. Wanatambua kipengele hicho kama grafolojia, ambacho wanakielezea kama mfumo wa uandishi. Leech na Short wanasema kuwa kupitia kwa matamshi, kiwango cha kisintaksia

katika sentensi hufikiwa, ilihali kupitia kwa grafolojia, kiwango cha fonolojia hufikiwa. Wanasisitiza kuwa tunapolisoma shairi bila kusikika, haimaanishi kwamba tumevisahau vipengele vya kifonolojia kama vile wizani, vina na vinginevyo. Vile vile wanasema kuwa katika usomaji wa riwaya, vipengele hivi vya sauti havijitokezi wazi, lakini huwa vipo na hutofautiana kutoka kwa mwandishi hadi mwingine. Wao wanaviainisha vipengele kadhaa vya kimtindo na wanakitaja kipengele cha

grafolojia kama mojawapo ya vipengele vya kimtindo.

Wanasema kuwa miongoni mwa vipengele muhimu vya kigrafolojia ni alama za uakifishaji, matumizi ya herufi kubwa, herufi za mlazo, kuepuka kutumia kikomo, tahajia pamoja na katuni.

Mawazo yao yanashadidiana na yale ya akina Ngara (1982) na Adegoju (2008) ambao wanasema kuwa hivi ni vipengele vya kigrafolojia katika maandishi na huwa na athari fulani kwa msomaji. Leech na Short (weshatajwa) wanasema kuwa ile hali ya kuligawanisha neno

kinyume na othografia ya neno hilo, na kuyaandika maneno bila nafasi za kiothografia ni dhahirisho kuwa dhana ya kigrafolojia imesheheni katika matini. Kulingana nao, vipengele hivi vinapotumiwa na mwandishi, huwa vinachangia katika kuimarisha uchimuzi kwenye matini.

Alo (1998) ameviainisha vipengele kadha vya kintindo vikiwemo fonolojia (sauti na athari zake), leksia (uteuzi na matumizi ya maneno), sarufi (muundo wa neno na sentensi), semantiki (maana), grafolojia (mfumo wa uandishi) na pragmatiki. Anasema kuwa grafolojia ni tawi la isimu ambalo hushughulikia uhakiki wa matini jinsi yalivyo, huku likizingatia muundo na sura ya maneno na vipengele vyovyote vya kiothografia.

Ogunsiji (2007) anavitaja vipengele mbalimbali vya kigrafolojia vikiwemo herufi kubwa, matumizi ya maandishi ya mlazo pamoja na matumizi ya viakifishi. Anasema kuwa, pia kuna uwezekano wa mwandishi kuepuka kukitumia kiakifishi chochote kama vile kikomo inapohitajika, pamoja na kukiuka mofolojia ya maneno, na hivyo basi kuibuka na msamiati ambao haukuendelezwa ipasavyo au ambao ni wa kigeni.

Kwa mawazo ya akina Leech na Short (weshatajwa), herufi kubwa katika matini hudhirisha matumizi ya mojawapo ya vipengele vya kigrafolojia. Wamitila (keshatajwa) anasema kuwa si ajabu kwa mwandishi wa riwaya kuwa na sentensi ambazo ni za neno moja au zile ambazo huanza kwa maneno yasiyokuwa ya kawaida. Anaendelea kutueleza kuwa, pia si ajabu kuiona kazi ya fasihi ambayo inapuuza kanuni za kimsingi za upangaji wa aya.

Kwa maoni yake, kuna uwezekano wa kazi za riwaya za kisasa kuwa na sifa za uakifishaji na uendelezaji wa maneno ambao si wa kawaida.

Wamitila (2008) anasema kuwa mtindo huu umekolea sana katika tanzu za kifasihi za kisasa, na hii ni ishara kuwa vipengele vya kigrafolojia vinatumika katika ujenzi wa tanzu hizi, kwa hivyo uhakiki kamili wa kazi hiyo huibua dhana ya uchimuzi ambayo mwandishi hunuia kuifikia anapotumia vipengele hivyo. Mawazo ya wataalamu hawa yalitupa mwelekeo mwafaka kuhusu dhana na dhima ya grafolojia ambayo ilikuwa malighafi ya utafiti. Kwa hivyo ni wazi kusema kuwa maana katika matini hupenyeza viwango vyote vya lugha, na uhakiki wa riwaya za kisasa ni vyema uangazie vipengele vya kigrafolojia.

Crystal (2003) anasema kuwa dhana ya grafolojia inahusu mfumo wa maandishi katika lugha. Anataja grafolojia kama mojapo ya matawi ya isimu inayojihusisha na uandishi na upigaji chapa kama mfumo wa ishara kwa kutumia teknolojia yoyote. Dhana hii yaweza kutumia teknonojia ya awali, kama vile kalamu na hata ile ya kisasa kama vile skrini ya kielektroniki. Chukwu (keshatawa) anataja viakifishi kama mojawapo ya vipengele vya kigrafolojia ambavyo hutumika katika uandishi. Anasema kuwa ni alama za mwandiko zinazoonekana, ambazo hutumika kirasmi katika mwambatano wa maandishi kinasaba.

Kwa mujibu wa Crystl (2003), alama hizi hazitumiki tu kwa kuzingatia kaida zilizozeleka bali hutekeleza dhima ya mwandishi kimawazo na kwa hali hiyo kuendeleza upekepeke wa

mwandishi kimtindo. Anasema kuwa dhana ya viakifishi inahusu matumizi ya alama hisi, ving'ong'o, vistari vifupi, alama za kunukuu, vinyota, udondoshaji, mabano, koma, koloni, semi-koloni, kikomo pamoja na viulizi. Kulingana naye, uwasilianaji kimaandishi huwa na vipengele vya kisarufi ambavyo hujumulisha mofimu, neno, vishazi, vifungu na sentensi vinavyotumika kusimba ujumbe.

Crystal (2003) anaendelea kusema kuwa kisemantiki, vipengele hivi huwa na ujumbe unaohusu ulimwengu lakini kimfumo, huzingatia sintaksia ya lugha husika. Kwa mujibu wake, viashiria na viashiriwa vya kigrafojia vinapopangwa kuwasilisha ujumbe, haviwezi kuibua maana bila kupambwa na viakifishi na mwandiko. Anasema kuwa viakifishi vinapotumika vyema na mwandiko katika matini, vinazua dhana ya matumizi ya madaha, ufungamano na ubembelezi katika kazi. Anasisitiza kuwa matumizi ya viakifishi, pamoja na vipengele vingine vya uchapaji humfafanua mwandishi mwema kimtindo.

Waldhorn na Zeiger (1980) wanasema kuwa viakifishi ni muhimu katika uandishi ingawa watu wachache wanaelewa mchango wa vipengele hivi. Edgar Alan Poe akirejelewa katika Ezugu (2001) anasema kuwa mwandishi yeyote anayepuza viakifishi katika uandishi wake huwa anaiharisha kazi yake pakubwa kwa kuzua utata kwa vile huwa anaiweka katika hali ya kutoeleweka.

Edgar Alan Poe (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa viakifishi ni alama za mwandiko ambazo kwa utaratibu fulani, hujumulishwa katika matini kwa kuzingatia kaida za

kimatumizi na hufaulisha dhima ya mwandishi ya kuwasilisha mawazo yake. Anaendelea kutufahamisha kuwa viakifishi huzua upekepeke wa mwandishi kimtindo katika matini kutegemea matumizi mema.

1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya kimtindo iliyoasisiwa na mwananadharia Baally (1909) na kuendelezwa na Jakobson (1958) na Halliday (1971). Hata hivyo mawazo ya waitifaki Short na Leech (1981) yalizingatiwa. Leech (1969) analezea kuwa nadharia ya kimtindo inatilia mkazo umuhim wa lugha kama chombo kinachomwezesha msanii wa kazi ya fasihi kuwasilisha ujumbe wake.

Kwa mujibu wa Crystal na Davy (1969), dhana ya kimtindo inaweza kuchanganuliwa kwa mitazamo minne. Kwanza kabisa, wanasema kuwa dhana hii yaweza kufasiriwa kama tabia ya mwandishi. Hii inatokana na uzoovu ambao msanii hudhihirisha katika matumizi yake ya lugha kuwasilisha ujumbe wake. Wanasema kuwa kila mwandishi hudhihirisha upekee wake katika kuiendeleza kazi yake, na upekee huo humtambulisha miongoni mwa wenzake.

Watalaam hawa Crystal na Davy (weshatajwa) pia wanaibuka na mtazamo wa kiitikadi katika kuelezea dhana hii. Kulingana nao, kila wanajamii wanao falsafa zao za kimtindo za kuwasilisha na kuendeleza ufundi wao. Falsafa hizo zinawiana na vipindi vya nyakati

mbalimbali na jinsi lugha ilivyotumika wakati huo. Kwa mfano kwa sasa nchini Kenya, matumizi ya lugha ya Sheng imekithiri miongoni mwa vijana, jambo ambalo halikuwepo miongo mitatu iliyopita. Wameshughulikia viwango mbalimbali vya kimtindo katika isimu ambavyo vyaweza kuangaziwa kama achano la kimtindo kati ya isimu na fasihi.

Crystal na Davy (weshatajwa) wanaibuka na mtazamo wa kiisimu-jamii katika ufafauzi wao wa dhana hii ya kimtindo. Kulingana nao, kazi ya fasihi huwasilishwa kwa mkundi mbali mbali ya kijamii na ufasiri mwaaka hutegemea tabaka ambalo kazi hiyo imewasilishwa.

Mwisho, wanasema kuwa dhana hii ya kimtindo huhitaji uelewa mpana kwa vile inahusu matumizi ya tamathali mbalimbali ambazo zaweza kuwa na maana fiche. Wanakubali kuwa kwa muda mrefu, pengo limekuwepo kati ya mchango wa isimu kwenye ujenzi wa utanzu wa riwaya na pengo hili limetokana na miundo hafifu ambayo wanaisimu wameshikilia katika tahakiki zao, huku wakiuelekeza uzito mwingi katika ujenzi na uhakiki wa utanzu wa ushairi. Hata hivyo, kwa sasa wanaisimu wengi wameweza kubadilisha mitazamo yao kuhusu vipengele vya kiisimu na hivyo basi kuzalisha dhana mpya ya kimtindo ambayo imewapa wanaisimu na wahakiki wa kifasihi fursa ya kutangamana na kuwa na mtazamo mpya kuhusu riwaya.

Kwa mujibu wa Leech na Short (weshatajwa) kwa sasa kunazo mbinu na dhana mpya za kiisimu ambazo zimeboresha utafiti na mtazamo kuhusu uhakiki bora wa utanzu wa riwaya. Wanasema kuwa kwa muda mrefu vipengele vingi vya kimtindo, kama vile vipengele vya

kigrafoloja vimepuuzwa katika uhakiki wa riwaya ilihali vina umuhimu mkubwa katika ujenzi wa utanzu huo. Kulingana nao, nadharia ya kimtindo yaweza kulinganishwa na utalii wa mwanaisimu na mhakiki, ambako isimu itajitokeza kama njia itakayomwezesha mtalii atambulike kimazungumzo.

Kwa mujibu wa akina Leech na Short (weshatajwa), lugha inajitokeza katika miktadha ya kibunifu na isiyobunifu. Wanatambua na kulinganisha lugha tambuzi za kanuni ya adhabu iliyokubalika na wanajamii. Kulingana nao, lugha inavyo viwango vitatu katika mfumo wake vyenye uhusiano wa karibu ambavyo ni semantiki, sintaksia na fonolojia. Wanasema kwamba dhana ya kimtindo huzuka na lengo la kuelezea tukio fulani na kwamba fasihi kimtindo hulenga kudhihirisha uhusiano uliopo baina ya lugha na jukumu la kiujumi, hivyo basi kuhalalisha welewa katika uhakiki.

Kulingana na mtazamo wao, Leech na Short (weshatajwa) wanasema kuwa lugha huchukuliwa kama njia mojawapo ya kuwasiliana kirasimi na kisasa. Wao wanashikilia kuwa katika maandishi, vipengele vyote vinavyotumiwa, viwe vya kiisimu au visiwe huwa vimebeba ujumbe fulani ambao unastahili kuangaziwa kiundani ili msomaji aweze kuupokea ujumbe ambao mwandishi alilenga kuuwasilisha. Kwa mawazo yao, mambo manne hujitokeza wazi kuhusu nadharia ya kimtindo; kwanza kutokana na dhana ya kimtindo, tabia ya mwandishi inabainika waziwazi, na pili ni kwamba tabia hiyo huchukuliwa kama utamaduni wa mwandishi huyo kwa vile itampa upekee na hivyo basi mawazo yake yatahitaji uhakiki mwafaka. Tatu, wao wanasema kuwa itategemea ni jamii ipi ambamo

dhana hiyo ya kimtindo itatumika na mwisho, wanataja ujuzi wa msomaji wa kazi ya fasihi kuweza kuifasiri kazi hiyo kama alivyolenga mwandishi.

Kulingana na Leech na Short (weshatajwa), kwa vile mojawo ya sifa bainifu ya riwaya ni kuhifadhiwa kimaandishi, kiwango ambacho ni muhimu ni kile cha grafolojia ambacho kinahusu mfumo wa uandishi.

Utafiti huu ulichunguza vipengele vingi vya kiisimu, hususan viakifishi ambavyo vimepuuzwa katika ujenzi na uhakiki wa riwaya kimtindo na kimuundo ilihali vina umuhimu mkubwa katika uhakiki wa utanzu huu.

1.8.1 Dhana ya Mtindo na Kimtindo

Sehemu hii inaangazia dhana ya mtindo na kimtindo katika muktadha wa riwaya teule. Mtafiti anaanza kwa kutoa fasili mbalimbali kuhusu dhana ya mtindo na kimtindo kama wavyoelezea wataalam. Hii inafanyika kutokana na changamoto zinazotokana na matumizi ya dhana hizi tofuti zinazoshabihiana katika utendakazi. Wataalam mbalimbali wakiwemo Leech na Short (weshatajwa) wanakubaliana kuwa dhana ya mtindo ni pana sana na kwamba inajitokeza katika shughuli zote maishani mwetu kama vile katika ujenzi, fasihi, tabia, isimu miongoni mwa taaluma nyinginezo. Utafiti huu ulichanganua dhana ya mtindo na kimtindo kiisimu na kifasihi huku uzito ukielekezwa katika mchango wa vipengele vya kigrafolojia hususan viakifishi katika uandishi wa riwaya teule.

Fasili nyingi zimetolewa na wamaisimu wengi wakiwemo Buffons (1930) kuhusu dhana ya mtindo. Wote wanakubaliana kuwa mtindo katika matini ndiyo makutanio ya uhakiki wa fasihi na uchanganuzi wa isimu. Wanasema kuwa kazi ya fasihi hudumu kupitia kwa mitindo iliyotumika katika kuiendeleza, na mitindo hiyo hubeba ujumbe mwingi kumhusu mwandishi mwenyewe. Wanaendelea kusema kuwa ili tuweza kuchanganua mtindo katika matini, ni lazima tuvichanganue vipengele vya kintindo ambavyo vinatumika na mwandishi vikiwemo vile vya kigrafolojia kama vile viakifishi, matumizi ya maandishi ya milazo, herufi kubwa, herufi nzito, katuni iongoni mwa vipengele vya kigrafolojia.

Kwa mujibu wa Coombes (1953), mtindo katika matini hujengeka kutokana na vigezo kadha vikiwemo uteuzi wa maneno, uradidi wa maneno na hata uvunjaji wa kaida za lugha husika pamoja na ukiukaji wa othografia ya maneno ambayo mwandishi hutumia katika kazi yake. Katika kufanya hivyo, mtindo huchukuliwa kama njia ya kuonyesha jinsi kazi ilivyoandikwa au kuendelezwa.

Leech na Short wanasema kuwa baadhi ya wanaisimu wanaonelea kuwa dhana ya mtindo inahusika na mambo yafuatayo;

- i) Uchunguzi wa uhusiano kati ya lugha na fikira. Katika mawazo haya, inajitokeza wazi kuwa lugha hutekeleza majukumu mawili. Hutumika kuwasiliana na pia kuelezea fikira za mtumiaji lugha.

- ii) Uchunguzi wa dhima ya lugha kiujumi. Mtazamo huu unaonelea kuwa mtindo ni urembo ambao mwandishi anauzingatia katika kazi yake na kwa kufanya hivyo, urembo huo humpa mwandishi huyo upekee.

Katika monografia yake, Enkvist anayerejelewa kwenye Khaled (2012) anazua mitazamo mbalimbali kuhusu dhana ya mtindo, ambayo watalaam wengine wanakubaliana naye. Anasema kuwa mtindo ni uamuzi wa mwandishi kuhusu jinsi atakavyoiwasilisha kazi yake. Kwa maoni yake, tunaweza kukubaliana kuwa mtindo ni tabia ya kipekee anayodhihirisha mwandishi fulani kupitia kwa maandishi yake ya kipindi fulani.

Leech na Short (weshatajwa) wanatahadharisha dhidi ya kuboea tu katika ufafanuzi wa dhana hii kwa vile huenda ikamuathiri msomaji visivyo na wanapendekeza kwamba ni bora ikiwa mtazamo ulioshikiliwa na wanamiundo kuhusu uhakiki wa matini unaoweka msisitizo kwa uhakiki wa viashiria na viashiriwa vya lugha iliyotumika katika uandishi.

Wamitila (2008) anasema kuwa mtindo hujumulisha zile mbinu zote ambazo mwandishi atazitumia katika kufaulisha na kuwasilisha ujumbe wake. Anaendelea kusema kuwa ni jumla ya vipengele ambavyo mwandishi atavifungamanisha katika kuwasilisha ujumbe. Katika kufanya hivyo, mtindo huo huweza kuchukuliwa kama tabia ya mwandishi huyo.

Kutokana na mchango wa watalaamu hawa, inadhihirika wazi kuwa dhana ya kintindo inahusu jinsi mwandishi anavyoweza kuiwasilisha kazi yake kwa njia ambayo anaifurahia

mwenyewe. Kwa hivyo, kigezo muhimu katika ufafanuzi wa dhana hii ni ‘jinsi’ ya kuiandika kazi. Dhana ya kimtindo vilevile imeshughulikiwa na wataalam mbalimbali wakiwemo Galperin (1981), Zhukovska (2010) miongoni mwa wengine na wote wanatueleza kuwa, dhana ya kimtindo ni mojawapo ya matawi ya isimu, ambayo huchunguza mfumo mzima wa kujieleza katika lugha fulani.

Galperin (1981) anasema kuwa lugha ni ngazi ya viwango kadha na kila kiwango huichunguza lugha kivyake. Kulingana naye, dhana ya kimtindo huchunguza vipengele vya kipekee ambavyo huibua maana dhanishi. Pia dhana ya kimtindo huchunguza matini fulani na lengo la kuibuka na diskosi mwafaka kwa kutegemea jinsi vipengele hivyo vilivyopangwa na kuibua maana kipragamatiki.

Galperin (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa dhana hii hujitokeza katika matawi yote ya lugha ambayo ni fonetiki, mofolojia, sintakasia na leksia. Kulingana naye, matawi haya yote yanajihusisha na vipengele vyote vya lugha na jinsi vinavyoingiliana na kuchangiana katika kufaulisha mawasiliano. Anatupa vigezo vinavyotumika katika kuainisha dhana ya kimtindo. Vigezo hivi ni pamoja na dhima, sifa, mbinu za utafiti na mada inamotafitiwa. Kutokana na utaratibu huo, kunaibuka aina kadha za kimtindo.

Kwa mujibu wa Galperin (keshatajwa), kila mojawapo ya aina ya kimtindo hujishughulisha na vipengele fulani vya lugha na huwa na dhima ya kuendeleza mawasiliano. Uainisho huo uliongozwa na mihimili miwili ifuatayo;

- i) Mhimili wa kujitokeza kwa lugha katika harakati mbalimbali. Mhimili huu umetokana na falsafa ya mwanamiundo Ferdinand de' Saussure ambaye alieleza lugha kama tawi linalodhihirisha mifumo ya ishara ambayo huongozwa na sheria fulani. Mhimili huu unaigawa dhana ya kimtindo katika makundi mawili, ambayo ni lugha kimtindo na mhadhara kimtindo. Lugha kimtindo huangazia vipengele vya lugha visivyoweza kubadilika, ambavyo vimo katika matini kama vile viakifishi, ilihali mhadhara kimtindo hujishughulisha na vipengele vya lugha katika muktadha wa matini kama vile kiimbo, shaddaa miongonimwa vingine.

- ii) Mhimili wa lugha kimaelezo. Mhimili huu unaigawa dhana ya kimtindo kwa vikundi viwili vya isimu na fasihi. Isimu kimtindo huchunguza lugha katika muktadha wa mazingira na umilisi wa mtumiaji lugha. Gaperin (keshatajwa) akirejelea fasihi kimtindo, anasema kuwa hii huchunguza fasihi kutokana na athari za kiuajumi. Anaendelea kutueleza kuwa, mhimili huu unazua dhana nyingine ya uandishi kimtindo. Uandishi kimtindo unatokana na mielekeo, itikadi na kazi zingine ambazo huenda mwandishi alizisoma, miongoni mwa athari ambazo humdhibiti katika uandishi wake.

Kulingana na Galperin (1981), mwandishi anapoendelea kuathirika kimtindo, athari hizo pia humfikia msomaji katika upokezi. Anasema kuwa dhima ya msomaji katika hali hii ya upokezi huathiriwa, na athari hiyo hujulikana kama uchimuzi. Dhima ya kimtindo katika muktadha huu huwa ni kuwasiliana kwa kutumia vipengele vyote vya lugha.

Mwananadharia wa kimtindo Bally, akirejelewa katika Taylor (1980) anapendekeza kuwa ni vyema ikiwa dhana ya kimtindo itaangaliwa kwa kuihusisha na tafiti zinazoelekezwa kwa elementi za lugha, na jinsi lugha hiyo inavyotekeleza dhima yake katika jamii. Hata hivyo Leech na Short (weshatajwa) wanaonelea kuwa mawazo ya Bally kuhusu dhana ya kimtindo hayakuelezea jinsi mwandishi anavyoweza kutoa hisia zake kuhusu tukio fulani, bila kuzifungamanisha na maana.

Bally anahitimisha mawazo yake kwa kusema kuwa dhana ya kimtindo ni vyema ivihusishe vigezo vyote vya uwasilishaji ujumbe; vile vinavyooneka na vile ambavyo hufikiriwa kubeba ujumbe wowote katika mawasiliano. Baada ya kuchochewa na mawazo ya Bally, Spitzer, mwananadharia wa kimtindo wa kisasaa anasema kuwa, njia ya pekee ambayo msomaji anaweza kuyapokea mawazo yaliyo ndani ya mwandishi ni kwa kuisoma kazi ya mwandishi huyo, kwa zaidi ya mara moja, huku msomaji akidhihirisha utulivu bila wasiwasi wowote.

Widdowson (1975) anaielezea dhana ya kimtindo kama sehemu ya isimu ambayo huzingatia sana mabadiliko katika matumizi ya lugha. Anaendelea kusema kuwa dhana ya kimtindo

hujitokeza tu kati ya isimu na uhakiki wa kifasihi, na hivyo hujenga muungano kati ya vipengele hivyo.

Wakichangia, Leech na Short wanasema kuwa dhana ya dhana ya kimtindo ni kuelezea uhusiano uliopo kati ya lugha na jukumu lake la kiujumi. Wao wanapendekeza kuwa ili kuelewa dhana ya kimtindo, ni vyema kujiuliza swali la “kwa nini? “ , na “ kwa njia ipi? ” kuliko kujiuliza swali la “ nini ? ”. Ngara (1982) ameshughulikia dhana ya kimtindo katika lugha kiundani na kuainisha viwango mbalimbali ambamo inajitokeza. Anataja kiwango cha maandishi ambacho hujumulisha matumizi ya vibonzo, rangi tofautitofauti, alama zinazochapishwa, viakifishi, na aya katika maandishi.

Utafiti huu ulijifunga katika kiwango cha maandishi kwa vile uliihakiki riwaya, na mchango wa Ngara uliunufaisha kwa mapana kwa vile ulilenga kuchunguza vipengele vya kigrafolojia vilivyotumika riwayani. Mohamed (1995) anasema kuwa dhana ya kimtindo inahusu namna ya kuitumia lugha ili kuweza kuufikia kwa ukamilifu maana au ujumbe unaotakikana kutolewa, na mara nyingine kuifikia maana au ujumbe huo pamoja na taathira fulani kama kipengele cha ziada katika matumizi ya lugha. Hata hivyo, ni vyema kubainisha kuwa lugha inavyo viwango mbalimbali na kile ambacho utafiti huu ulijihusisha nacho ni kiwango cha kimaandishi na hususan alama za viakifishi.

Mohamed (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa dhana ya kimtindo ni kipengele cha matumizi lugha ambacho huwa na maana nyingi. Kulingana naye, dhana hii humhusu mtu

binafsi kama mtumizi lugha au watumizi wa lugha katika kikundi fulani cha uandishi. Kwa mawazo yake, dhana ya kimitindo inaweza kuwa na kielelezo cha pande tatu ambazo ni mtumizi lugha, lugha yenyewe na miundo na maumbo yake, na hulenga kuendeleza mawasiliano katika uwanja au muktadha fulani wa matumizi lugha.

Kwa maoni ya Mohamed (keshatajwa), wazo na lugha ni dhana zisizoweza kutenganishwa na vina uhusiano kama ule wa kuku na yai, uhusiano ambao ni vigumu kubaini ni kipi kimekuja mwanzo. Kwa hivyo ni dhahiri kuwa uhakiki wa matini kimitindo ni vyema uangazie mwandishi na msomaji. Hii inatokana na maoni kuwa waandishi wa matini huendeleza kazi zao kwa aina mbalimbali za kimitindo, na hivyo basi wao huibuka na upekee fulani wanapoandika.

Mohamed (keshatajwa) anasema kuwa jinsi mwandishi anavyojichagulia maneno pamoja na anavyoyapanga kimaandishi akizingatia vipengele vingine kama vile urefu wa sentensi, maumbo ya sentensi hizo, toni miongoni mwa vipengele vingine vya uandishi, upekee wake huibuka kimitindo. Kulingana naye, kwa vile maneno tofauti huibua maana tofauti akilini mwa mwandishi, uchaguzi huo wa maneno ni muhimu katika kuudhibiti uitikio wa msomaji. Anaona kuwa uteuzi huo wa maneno ni muhimu kwa hadhira, pamoja na mazingira wanamowekwa na mwandishi.

Kwa mujibu wa Mohamed (keshatajwa), dhana ya kimitindo katika uandishi pia huibua toni, kutegemea muktadha ambamo sentensi hujitokeza na ufasiri wake kwa njia iliyo sawa.

Anasema kuwa, kuwepo kwa aina mbalimbali ya kimitindo na jinsi inavyodhihirika katika uhakiki kimatini ni ishara kuwa kunavyo vipengele mbalimbali vya lugha ambavyo huchangia katika uimarishaji wa kazi ya fasihi, kama tulivyodhihirisha katika utafiti kwa msingi wa riwaya ya *Mkamandume*.

Kwa mujibu wa Meyer (1997), vipengele vya kuonwa katika matini hususan riwaya huwa na mchango mkubwa katika fasihi. Anaviita vipengele hivi vipengele vya kigrafolojia ambavyo anasema kuwa, huchangia katika uimarishaji wa uchimuzi katika matini. Anasema kuwa vipengele vya kigrafolojia ni vingi na hujumulisha viakifishi, matumizi ya herufi kubwa, herufi nzito, herufi za milazo, michoro mbalimbali, katuni na hata fonti mbalimbali za uandishi. Anasema kuwa vipengele hivi vinaweza kuchangia katika ukiukaji wa mofolojia ya maneno, uibukaji na maneno yasiyo ya kawaida, kando na kuyaendeleza maneno hayo bila kuzingatia nafasi za kiothografia. Kwa kufanya hivyo, mwandishi huibuka na upekee wake kimitindo.

Mawazo haya yaliuboresha utafiti huu kwa vile yaliipa mada ya utafiti mwanga kuhusu jinsi lugha inavyofinyangwa na wandishi katika jitihada zao za kuyaafikia maazimio yao pamoja na kujitambulisha. Bradford (1997) anasema kuwa dhana ya kimitindo ni telezi na yenye kusererereka, ingawa inatuwezesha kutambua na kutaja vigezo tofauti vya matini kifasihi na kubainisha ainasafu na miundo mbalimbali ya fasihi.

Bradford (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa tunapotumia au kuitikia lugha katika ulimwengu wetu wa uelewa wa maana ya maneno fulani, maana ya maneno hayo huongozwa na vigezo vingi vya kimuktadha na kimazingira. Bradford anaendelea kusema kwamba, lugha hutuwezesha kueleza kwa ufasaha mfuatano wa matukio, uamuzi, miitikio na matukio huku kipengele cha kimtindo kikichangia katika kuendeleza jukumu la kipragmatiki na dhima.

Bradford (keshatajwa) anaainisha dhana ya kimtindo kwa njia mbili; maandiko, ambayo huangazia vigezo vya kimtindo katika matini fulani kifasihi kama zalisho la umoja kijarabati na ukamilifu. Kutokana na uainisho wake, ingawa wizani nikipengele cha lugha zungumzwa zote, lakini kipengele hiki cha lugha kinapowekwa pamoja ili kutawala jengo la matini, matini hiyo huchukuliwa kama fasihi.

Njia ya pili ambayo Bradford anayoitazama dhana hii ni ya kimuktadha, ambayo anasema kuwa hii inahusu jinsi matini inavyohusishwa na muktadha inamotumika. Wazo la Bradford (1997) kuhusu dhana ya kimtindo kama maandiko katika matini liliudhibiti na kuufanikisha utafiti huu kwa vile utafiti ulilenga maandishi.

Kulingana na Mbatiah (2001), dhana ya kimtindo inahusu jinsi mtunzi wa kazi ya sanaa anavyotumia lugha kujieleza. Anaendelea kutueleza kuwa uchanganuzi wa kazi ya kifasihi kimtindo unahusu mambo kama vile uteuzi wa msamiati, tamathali za semi zilizotumiwa, miundo ya sentensi, aya, beti miongoni mwa vipengele vingine, na kwamba dhana hii

hujumlisha vipengele vyote vya lugha. Hata hivyo, ni vyema ibainike wazi kuwa utafiti huu ulinuia kuchunguza dhana ya kimtindo kimandishi. Mawazo yake yalituchochea kuangazia vipengele vingi vya kigrafolojia katika isimu ili tuweze kuibuka na matokeo ya kutegemewa.

Verdonk (2002) anasema kuwa dhana ya kimtindo inahusu uhakiki tofauti wa lugha kwa kuzingatia shabaha na athari zake katika matini. Kulingana naye, kinyume na yalivyo mazoea katika utanzu wa ushairi ambapo washairi wanaifinyanga lugha kwa manufaa yao, mtindo huo umeweza kupenyeza katika utanzu wa riwaya ya kisasa. Anasema kuwa maandishi ya riwaya ya kisasa yanadhihirisha matumizi mengi ya vipengele vya kigrafolojia ambavyo vina athari ya kisaikolojia kwa msomaji inayojulikana kama uchimuzi. Anataja vipengele vingine vya kigrafolojia ambavyo ni pamoja na usambamba katika taipografia ya matini, sauti, uchaguzi na mpangilio wa maneno, lugha na muundo wa sentensi.

Verdonk (keshatajwa) anasema kuwa vipimo vingine vya kimtindo ni pamoja na uradidi wa baadhi ya vipashio vya kiisimu na uvunjaji wa sheria za kiisimu kwa ujumla katika matini. Kulingana naye, dhana hii ya kimtindo haiibuki katika ombwe tupu bali huwa ni zalisho la mwaandishi, na msomaji anahitaji kuzingatia muktadha wa kazi hiyo ili aifikie shabaha na athari ya mwandishi. Akizungumzia muktadha, anatumieza kuwa aina mbili za muktadha hujitokeza katika hali hii ambazo ni muktadha wa kiisimu na muktadha usio wa kiisimu.

Kulingana na Verdonk, muktadha wa kiisimu hujumlisha mazingira ya kilugha ndani ya matini kama vile taipografia, sauti, maneno, vifungu vya maneno na sentensi ambazo

zinahusika na ufasiri wa vipengele vingine vya kiisimu, ilihali muktadha usio wa kiisimu unahusu vipengele vya nje, vinavyomzingira mwandishi ambavyo haviwezi kutambulika katika uhakiki wa matini.

Mehmood na wenzake (2014) wanaifafanua dhana ya kimtindo kama taaluma inayojihusisha na ufasiri wa matini na utofauti wa matumizi ya lugha. Wanaendelea kusema kuwa ni sayansi ya uchanganuzi lugha ambayo hurejelea viwango vyote vya lugha, vikiwa ni pamoja na fonolojia, mofolojia, sintaksia na leksia, na kwamba dhana hii hutumika sana katika taaluma ya fasihi.

Mchango wa wataalam hawa ulikuwa wa manufaa mno katika kuuwekea utafiti huu msingi mwema. Aidha, dhana hizo za mtindo na kimtindo ziliweza kubainika wazi na michango ya dhana hizi katika riwaya teule uliweza kutambulika.

1.8.2 Mihimili muhimu ya nadharia ya kimtindo

Utafiti huu uliongozwa na mihimili ifuatayo kwa maoni ya akina Leech na Short (weshatajwa);

- i. Riwaya huwasilishwa kimaandishi, na kupitia kwa njia hii, matumizi ya vipengele vya kigrafolojia kimtindo hujitokeza kama njia bainifu ya kumtambulisha mwandishi.
- ii. Matumizi ya vipengele vya kigrafolojia riwayani humuathiri msomaji.
- iii. Vipengele vya kigrafolojia huimarisha uchimuzi katika riwaya.

- iv. Mwandishi wa riwaya huweza kuifinyanga lugha anayoitumia na kuibuka na lugha mpya katika kazi yake.

Utafiti huu uliongozwa na mihimili iliyotajwa huku kila mhimili ukishughulikiwa kiundani kwa minajili ya riwaya teule ya *Mkamandume*. Wamitila (keshatajwa), anasema kuwa mkabala unaosisitiza nafasi ya msomaji katika kuivyaza maana ya kifasihi hujengwa katika imani ya kwamba matini ya kifasihi haina maana funge na thabiti, na kwamba maana hujitokeza tuu iwapo msomaji ataisoma kazi hiyo kisha aipe fasiri ndiposa aibuke na maana.

1.9 Mbinu za utafiti

1.9.1 Muundo wa utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Utaratibu wa utafiti huu wa kimaelezo huchunguza sifa bainishi katika jambo lifanyiwalo utafiti jinsi lilivyo na kulirekodi. Data hukusanywa na lengo la kubainisha uhusiano uliopo baina ya vigezo vilivyopo. Kutokana na utaratibu huu, maelezo muhimu yaliweza kuzingatiwa kuhusu dhana za grafolojia na uchimuzi kimtindo katika uchapaji wa riwaya teule.

1.9.2 Mahali pa utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani, kwa hivyo ulihusu usomaji wa riwaya teule kwa kina miongoni mwa riwaya zingine, pamoja na majarida na hata kutafiti katika vyombo vingine

vya habari kama vile tovuti kwenye mtandao. Hii iliniwezesha kupata habari nyingi kuhusu mada ya utafiti pamoja na nadharia ya kimtindo ambayo iliongoza utafiti huu.

Utafiti wa kimaktaba huwa na utaratibu wa ukusanyaji data ambao hauleti data ya kitakwimu na katika hali ya kawaida, data yake huwa katika maelezo ya maneno, ufafanuzi na aya hugawika katika vikundi kutegemea dhana linganifu.

Kupitia njia hii ya utafiti, niliweza kutathimini vipengele vya kigrafolojia ambavyo mwandishi wa riwaya teule alivitumia huku athari yavyo ikibainishwa.

1.9.3 Sampuli lengwa

Sampuli lengwa katika utafiti huu ilikuwa riwaya ya *Mkamandume* kwa hivyo ni utafiti ambao ukijikita katika fasihi andishi na riwaya ya kisasa iliyochaguliwa kimakusudi. Mbinu hii ya usampulishaji kimakusudi huteua sampuli lengwa kwa kuzingatia misingi na malengo ya utafiti. Katika utafiti huu, niliteua fasihi andishi kimakusudi na riwaya ya *Mkamandume* kama sampuli mwafaka ya riwaya ya kisasa ili kuyaafikia maazimio yangu.

1.9.4 Mbinu za ukusanyaji wa data

Data ilikusanywa baada ya kusoma matini teule kwa kina, ambapo nilidondoa na kunukuu sehemu ambazo vipengele hivi vya kigrafolojia vilitumika na kuviainisha. Mbinu hii iliniwezesha kupata ujumbe wa kwanza uliyohusu mchango wa viakifishi kuhusu ujenzi wa riwaya ya *Mkamandume* kuunakili kama ulivyojitokeza bila athari zozote.

1.9.5 Uchanganuzi wa data

Data iliyokusanywa kutoka kwa riwaya ilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti. Data hii ilikuwa viakifishi ambayo niliweza kuviainisha kwa makundi matatu makuu; viakifishi vya neno, viakifishi vya ndani na viakifishi tamati. Baada ya uainisho huo, niliweza kuangazia vijisehemu vya kila kundi la viakifishi na kudhihirisha jinsi mwandishi alivyovitumia kukuza riwaya yake.

1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Data iliyochanganuliwa iliwasilishwa kwa njia ya kinaelezo ambamo nilidhihirisha namna grafolojia ni dhana muhimu katika ujenzi wa riwaya teule na jinsi inavyomuathiri msomaji. Matokeo ya utafiti huu yaliwalishwa kwa njia ya maelezo ambapo kwa muhtasari, mtafiti alidhihirisha jinsi viakifishi vilivyo vipengele muhimu katika ujenzi wa riwaya teule kwa kutoa mifano kwenye riwaya inayoonyesha matumizi ya vipengele hivyo na ufasiri unaotokana na matumizi hayo.

1.9.7 Kiishilio

Sura hii ya kwanza ilirejelea masuala ya kimsingi katika utafiti huu ambamo usuli, suala, maswali ya utafiti, malengo, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa nadharia pamoja na mbinu za utafiti zilirejelewa. Mawazo yaliyoangaziwa katika sura hii ndiyo yaliyokuwa msingi wa utafiti.

SURA YA PILI: RIWAYA YA KISASA

2. Utangulizi

Sura hii iliiangazia riwaya ya kisasa katika mazingira au miktadha ya Kimagharibi na Uswahilini. Aidha, misingi ya dhana ya riwaya, riwaya ya kisasa na riwaya ya kisasa ya Kiswahili ilianguziwa kwa upana. Mchango wa wataalamu mbalimbali uliangaziwa kuhusu dhana hizi ambao uliweza kuuwekea utafiti huu msingi mwafaka. Kwa mujibu wa Wamitila (2008), usasa riwaya unaainishwa kwa mtindo - mbinu za uwasilishi kama ndoto, mbinu rejeshi, ritifaa, mjadala nafsi miongoni mwa mbinu zingine na mbinu hizi huweza kuchimuzwa kwa kutumia vipengele mbalimbali vya grafolojia.

2.1 Dhana ya riwaya ya kisasa.

Mlacha na Madumulla (1991) wametoa maelezo kuhusu historia ya riwaya ulimwenguni na wanasema kuwa haina umri mkubwa, hasa inapolinganishwa na historia ya tanzu nyingine za fasihi andishi kama vile ushairi na tamthilia. Hata hivyo wanasisitiza kuwa mageuko ambayo utanzu wa riwaya umepitia yanadhihirisha ufanisi mkubwa na wa kustaajabisha. Licha ya kuwa ni utanzu ulioanza kwa unyenyekevu, kufikia sasa riwaya imedhihirisha upekee na uwezo mkubwa wa kuhimili mabadiliko, uvumbuzi, kueneza na kudhibiti matukio mengi katika jamii.

Ingawa chimbuko na maenezi ya utanzu huu umezua mijadala mingi, kuna mtazamo unaoshikiliwa na wengi kwamba utanzu huu uliibuka baadaye kihistoria kama mishabihiano ya kifasihi kudhihirisha usasa.

Usasa na riwaya ya kisasa ni dhana tepetepe. Mulokozi (1996) na Wamitila (2003) wameziainisha aina za riwaya na katika uainisho wao, wametaja riwaya ya kisasa. Kulingana nao, riwaya ya kisasa ni riwaya ya kimajaribio. Wanaielezea kama ile inayoujadili mkondo wa nafasi ya riwaya, iliyotungwa bila kuzingatia kanuni za kawaida za uandishi wa riwaya. Wanasema kuwa aina hii ya riwaya hutosheleza mahitaji ya karne hii na inawakilisha ukweli wa maisha.

Wamitila (2008) anaielezea riwaya ya kisasa kama ile inayowaangazia wanasiasa, ambayo inadhamiria kuyafichua mambo yanayotendeka kinyume na matarajio ya jamii. Maelezo haya yana uhusiano wa karibu na riwaya ya kidastopia inayoisawiri jamii isiyokuwa ya kawaida kwa wakati maalum, yani inayofikiriwa tuu. Hii ni jamii ambayo inaishi katika mazingira ambamo sheria za kawaida za kijamii zimebadilishwa kwa namna inayowafanya watu wengi kuishi maisha ya taabu yenye mateso mengi kama inavyodhihirika katika riwaya za *Walenisi* na *Mkamandume*.

Hata hivyo, wananadharia wa riwaya ya kisasa wanakubaliana kwamba, jinsi mfumo wa utaalamishaji ulivyoshika kasi kwa kuziondoa imani za kidini, utanzu huu nao pia uliweza kujiimarisha, huku masimulizi kama vile ya kibwege na fantasia yakiepukika. Kwa mujibu wa Bleiman na wenzake (2001), riwaya ya kisasa inawarejelea raia wa kawaida katika ulimwengu wa kihalisia. Anasema kuwa, jinsi Copernicus alivyozua mapinduzi katika taaluma ya kosmolojia, Miguel de Cervantes, Mme de Lafayette, Daniel Defoe, au Samuel Richardson ndio waasisi wa riwaya ya kisasa.

Kulingana na Bleiman na wenzake (weshatajwa), kando na mikakati ya uhalisia, riwaya ya kisasa ina sifa ya mikingamano na hukaidi uandishi wa kawaida. Wananadharia wa riwaya ya kisasa wakiongozwa na Joyce katika Parsons (2007) wanasema kuwa dhana ya usasa hudokeza wepesi wa kuhisi kwa misingi ya kijamii, kinyume na kipindi fulani bila kujifunga kwa kipindi fulani cha kihistoria. Wanaendelea kusema kuwa vigezo vya kimtindo na mifumo ni muhimu katika uhakiki wa riwaya ya kisasa, na kwamba kutokana na kufifia kwa athari za uhakiki mpya zilizoshika kasi miaka ya hamsini, kuna mtazamo mpya ambao riwaya za kisasa huangazia.

Kwa mujibu Bleiman na wenzake (weshatajwa), riwaya ya kisasa huzama sana katika masuala ya sayansi ya kijamii kwa muktadha wa matukio ya kihistoria na athari zake, pamoja na falsafa nyingi kinzani zinazojikita katika fikira za kisasa. Wanasema kuwa hii riwaya

inajihusisha na maisha ya ung'amuzi wa nafsi; iliyofichika na ile iliyopoteza fahamu na inaongozwa na uhalisia mpya.

Kwa mujibu wa wananadharia hawa, riwaya ya kisasa ilitangua mapatano na matarajio ya fasihi, huku ikikaidi taswira ya uhalisia, utambuzi na utambulisho mwanzoni mwa karne ya ishirini. Wanaendelea kusema kuwa riwaya hii si bora tu kwa ubunifu bali pia inachangia katika ufasaha na mapinduzi ya maendeleo ya uyaakinifu. Parsons (keshatajwa) anasema kuwa riwaya ya kisasa haiwezi kushughulikiwa bila mawazo ya akina James Joyce, Dorothy Richardson na Virginia Woolf.

Parsons (2007) anaendelea kusema kuwa ni vyema ikiwa utanzu wa riwaya ya kisasa utashughulikiwa kwa msingi wa mchango wa wananadharia hawa ambao wameirejelea mifumo ya uhalisia, mapatano kuhusu wahusika na utambuzi, jinsia, pamoja na dhana ya muda na historia. Kulingana naye, ufahamu kuhusu wananadharia hawa ndio msingi wa uelewa wa usasa na riwaya ya kisasa, na kwamba yeyote ambaye angependa kuelewa utanzu wa riwaya ya kisasa, basi hana budi kuzingatia mawazo yao.

Kwa mujibu wa Parsons (2007), wananadharia hawa wanatueleza kuwa mwanzoni mwa karne ya ishirini, kuliibuka mwamko mpya katika historia ya utanzu wa riwaya, kwa vile mijadala mingi iliendelezwa kutoka kwa waandishi na wakaguzi walioulizia jinsi mfumo na muundo wa riwaya ya kisasa ulivyoniua kuingiliana na umbo na uzoefu wa maisha ya kisasa.

Kwa maoni yao, wasomi wa riwaya ya kisasa huenda wakaichukulia kazi hiyo kama utunzi wenye mnyumbuko na mabadiliko kimuundo, kiasi cha kujumulisha mitindo mingi na hata tanzu zingine.

Parsons (2007) anasema kuwa wao wanaendelea kusema kuwa, miamko na uvumbuzi uliotekelwa na akina Darwin, Freud na Einstein miongoni mwa wanasayansi wengine katika karne ya kumi na tisa uliathiri pakubwa riwaya ya kisasa. Wananadharia hawa wanasema kuwa riwaya ya kisasa ni ile yenye siasa kali kirasmi, inayohimili uhalisia wa kiasili na yenye kudhihirisha ujitawala kiujumi. Kando na sifa wanazozitaja, wanasema kuwa ni vyema riwaya hiyo idhihirishe mfululizo wa matukio ya kiulimwengu ambayo usasa unaonekana kuyakaidi. Kulingana nao, ikiwa utunzi wa riwaya utazingatia mawazo haya, basi utatosheleza kuitwa riwaya ya kisasa.

Wanasisitiza kuwa ni jukumu la mwandishi wa riwaya ya kisasa kuihusisha kazi yake na changamoto zinazotokana na masuala ya kihusiano, kisiasa na kimaadili ya wakati wake, na pia kuitumia riwaya hiyo kama kipimo mwafaka cha kusuluhisha masuala hayo katika jamii. Kuhusu dhima ya riwaya ya kisasa, Wells akirejelewa katika Parsons (keshatajwa) anasema kuwa riwaya ya kisasa inalenga kutekeleza mapinduzi ya kijamii na kuendeleza mshikamano dhabiti wa kisiasa kwa uwezekano wote.

Kwa maoni yao, vipengele vikuu vinavyotambulisha riwaya ya kisasa ni uhalisia wa kisasa, uhusika na utambuzi, jinsia, nyakati na historia. Wakizungumzia kuhusu uhalisia, wanasema kuwa riwaya ya kisasa ni lazima iwe kiwakilisho cha maisha jinsi yalivyo sasa, kinyume na tendi za kirasimi ambazo ziliwaangazia majagina na ujabu wao tu. Watts anayerejelewa katika Parsons anaelezea riwaya ya kisasa kama ile ambayo imejengeka kwa misingi ya kikweli kulingana na tajriba ya kibinadamu, na kwamba inalenga kumpa msomaji matukio ya kikweli huku ikirejelea nyakati na mahala pa matukio, ambayo huelezwa kwa lugha inayofahamika.

Akizungumzia dhana ya ubinadamu, Watts anayerejelewa katika Parsons (2007) anasema kuwa ni pana na uhalisia huwa na mifumo mingi. Anaendea kusema kuwa mwandishi wa riwaya ya kisasa ni vyema azame katika matukio ya kiutangamano, kimaadili na changamoto zinazoenezwa na siasa kiwakati kama jinsi zilivyoanzishwa na mfumo wa kiviwandani na ubepari kwa ujumla. Kwa hali hii, riwaya ya kisasa inakuwa na dhima inayofahamika waziwazi.

Hata hivyo, ni vyema ifahamike wazi kuwa mawazo yanayoshikiliwa na wananadharia hawa yamejikita katika riwaya ya kisasa ya kimagharibi. Kwa hivyo ni vyema ifahamike kuwa riwaya ya Kiswahili ya kisasa haina uhusiano wowote na matini ya kidaistopia ya kirasimi ya kimagharibi. Kwa mujibu wa Gromov (2014), ni nadra kuipata kazi ya Orwell ya

kimavamizi, ya Huxley ya kijasiri au ya Zamyatin kuhusu nchi isiyokamilika yakirejelewa katika riwaya ya Kiswahili ya kisasa. Waandishi wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa huubuni ulimwengu wao kwa kuyatumia malighafi yao ya kiasili katika muktadha wa wahusika, mandhari, motifu miongoni mwa vipengele vingine.

Kulingana na Gromov (keshatajwa), historia ya riwaya ya kisasa ya Kiswahili inaanza kwa kuushughulikia utanzu wa riwaya wa Kiswahili hatua kwa hatua.

2.2 Msingi wa riwaya ya Kiswahili

Watalaam wengi wakiwemo Senkoro (1977) na Wamitila (2003) wanakubaliana kuwa riwaya ni kazi ya kinathari au kibunilizi ambayo huwa na urefu wa kutosha, msuko uliojengeka vizuri, wahusika wengi walioendelezwa kwa kina, yenye kuchua muda mwingi katika maandalizi na kuhusisha mandhari maalumu. Hata hivyo wanatofautiana kuhusu kigezo cha urefu kwa vile kulingana na Mphahalele anayenukuliwa na Mulokozi (keshatajwa), riwaya huwa fupi ikiwa ina kati ya maneno elfu thelathini na tano hadi elfu hamsini na huwa ndefu ikiwa itakuwa na maneno kati ya elfu hamsini hadi elfu sabini na tano. Kwa hivyo inadhihirika kuwa kigezo hiki cha urefu kinazua utata katika ufafanuzi wa riwaya.

Wamitila na Senkoro (weshatajwa) wanasema kwamba ikiwa kigezo cha urefu kitazingatiwa katika ufafanuzi wa riwaya, bila shaka idadi ya riwaya kwa ujumla itakuwa ndogo kwa vile

kigezo hiki hakitakubaliana na riwaya kama vile za Kezihahabi za *Nagona* na *Mzingile* kwa vile hazina idadi kubwa ya maneno. Wanapendekeza kuwa kigezo cha mchangamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa uzito na undani kwa mambo mbalimbali ya kimaudhui na kiufundi kizingatiwe katika ufafanuzi wa riwaya. Kulingana nao, kisa hiki huwa ni kirefu, urefu unaokiruhusu kutamba mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi kama apendavyo mwandishi.

Kulingana na fasili za watalaamu hawa, tunaweza kuifafanua riwaya kama masimulizi ya kibunifu ya kinathari yenye msuko au mpangilio fulani wa matukio au ploti inayofungamana na wakati au kusawiri wakati, na yenye visa vingi vinavyotendeka katika wakati fulani na yenye mawanda mapana ya mchangamano wa dhamira, visa na wahusika.

Watalaam hawa vile vile wametoa mawazo kuhusu riwaya ya Kiswahili, na wanakubaliana kuwa, ni lazima iwe riwaya iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Wanasisitiza kuwa lugha ya Kiswahili ni kigezo muhimu katika utambuaaji wa riwaya ya Kiswahili. Kulingana na Mulokozi (keshatajwa), asili ya riwaya ya Kiswahili imo katika tanzu asili za jamii za mwambao mwa Afrika Mashariki.

Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kuwa historia ya riwaya ya Kiswahili inafungamana na historia ya maendeleo ya jamii za mwambao mwa pwani ya Afrika Mashariki. Hii ina maana kwamba, mtu anapotaka kuelezea juu ya chimbuko la riwaya ya Kiswahili, ni vyema

kuyarejelea maendeleo ya jamii ya Waswahili wa Pwani, katika vipindi mbalimbali vya maendeleo yao kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni.

Hata hivyo ubishi unaibuka kuhusu chimbuko la riwaya ya Kiswahili. Kulingana na Ohly (1981), riwaya ya Kiswahili ilianza wakati Edward Steere alipozikusanya simulizi za wenyeji wa Unguja na kuzihariri mwaka wa 1870. Wapo wale wanaoshikilia kuwa riwaya ya Kiswahili ilianza robo ya kwanza ya karne hii ambapo kitabu cha *Mwaka katika Minyororo* (1921) kilipoandikwa.

Kwa mujibu wa Senkoro (keshatajwa), riwaya ya Kiswahili ya kwanza ilikuwa *Uhuru wa Watumwa*, utunzi wa James Mbotela iliyochapishwa mwaka wa (1934). Anaendelea kusema kuwa, riwaya hiyo ilikuwa na mandhari ya kuku huku Afrika Mashariki, kwa vile wahusika walikuwa Waswahili, na maudhui yaliwahusu Waswahili kwa ujumla. Kando na hayo, mwandishi wa riwaya hiyo James Mbotela alikuwa Mswahili bila shaka.

Hata hivyo madai haya yaliibua mjadala mkali, na yalipingwa na Kezilahabi (1980) na Shariff (1988). Hawa wahakiki walitofautiana kuhusu nani aliyekuwa Mswahili, huku Shariff akishuku ikiwa kweli riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* iliandikwa na James Mbotela. Kuna wengine wanaosema kuwa riwaya ya Kiswahili ya kwanza ilianza mwaka wa 1974 wakati Kezilahabi aliandika *Kichwamaji*.

Mlacha na mwenzake (1991) wanasema kuwa la muhimu kuzingatia tunapoizungumzia riwaya ya Kiswahili ni lugha inayotumika katika usimulizi huo, ambayo lazima iwe Kiswahili. Wanasema kuwa riwaya zilizotafsiriwa ni lazima ziangaliwe tu katika mchango wao wa kuiendeleza riwaya ya Kiswahili bali siyo kwamba ni riwaya kamili.

Mulokozi (keshatajwa) anasema kuwa ikiwa riwaya ya Kiswahili ya awali italinganishwa na tanzu zingine za awali, haitaonyesha maendeleo makubwa ya kupevuka, ingawa anagusia kuwa waandishi wa kazi hizi; *Ubeberu Utashindwa* (1971), *Kichwamaji* (1974), *Dunia uwanja wa Fujo* (1974) ni miongoni mwa waandishi wa kutajika wa riwaya ya Kiswahili, kwa vile kazi zao zinadhihirisha ubunifu mkubwa huku zikitofautiana na za wale waandishi wa awali ambao kazi zao zilijitokeza kama mkusanyiko wa masimulizi yasiyodhihirisha ubunifu wowote. Kwa njia nyingine, Mulokozi anatuashiria kuwa riwaya kamili ya Kiswahili ilianza miaka ya Sabini.

Kulingana na Verdonk (2002), Kezilahabi ni miongoni mwa wandishi ambao wamejitokeza na mtindo wenye athari za akina Thomas Mann na Albert Camus, wanaojumulishwa katika kundi la kidhanaishi, yani kundi la wandishi ambalo linatumia nafsi kama kigezo cha kuyapima malimwengu badala ya kuyatumia malimwengu kama kigezo cha kupima nafsi. Msingi huu kuhusu dhana ya riwaya na riwaya ya Kiswahili kwa ujumla ni muhimu kwa vile unatuwezesha kupata mwelekeo kuhusu mada tunayoishughulikia.

Watalaam pia wameweza kushughulikia umbo la utanzu wa riwaya na kuibuka na mawazo kuwa dhana ya grafolojia ilitumika katika ujenzi wa riwaya za hapo awali na kwamba siyo dhana mpya kutumika katika utanzu wa riwaya. Tukizirejelea riwaya za awali kama vile *Kusadikika* (1951), tunatambua kwamba mwandishi Shaaban Robert alitumia vipengele vya kigrafolojia kwa vile aliweza kuianza kila sura ya riwaya hiyo kwa neno zima lililoandikwa kwa herufi kubwa, kando na michoro inayodhihirika riwayani humo miongoni mwa vipengele vingine vya kigrafolojia.

Katika riwaya ya *Simu ya Kifo* (1965), Katalambulla alitumia vipengele vingi vya kigrafolojia kama vile alama za udondoshaji, maandishi ya *milazo* miongoni mwa vipengele vingine. Kwa mfano katika ile ripoti ya daktari kuhusu kifo cha Mzee Jacob, maandishi ya mlazo yamesheheni huku akitumia herufi kubwa na nzito kila mwanzo mwa sura. Mwandishi wa riwaya hii pai anayatumia maneno yenye herufi kubwa na nzito katikati mwa sentensi, anaitumia michoro mbalimbali katika ujenzi wa riwaya hiyo miongoni mwa vipengele vingine vya kigrafolojia.

Kwenye riwaya ya *Kisima cha Giningi* (1968), mwandishi Muhammed, S. A. alivitumia vipengele vya kigrafolojia kama vile deshi (-) katika kujenga kazi yake. Katika riwaya hiyo, pia maandishi ya *mlazo* yametumika kwa mapana kama vile kwenye barua ambayo Seif alimwandikia Bwana Msa. Anwani za sura zote kumi na mbili riwayani humo zimelazwa. Msamiati usioeleweka ambao mwandishi aliutumia pia umelazwa.

Marejeleo ya diwani ya *Utubora Mkulima* (1968), mwandishi Shaaban Robert bado ameuzingatia ule utaratibu wa awali kama ulivyozingatiwa katika diwani ya *Kusadikika* ambapo kila sura ya riwaya yake inaanza kwa neno lililoandikwa kwa herufi kubwa. Vipengele vingine vya kigrafolojia kama vile mlazo, herufi kubwa na nzito, viakifishi vimetumika vile vile.

Kwa hivyo inabainika wazi kuwa matumizi ya vipengele vya kigrafolojia si mageni katika utanzu wa riwaya, lakini katika kuangalia matumizi ya vipengele hivi kwa jicho la ndani huku miktadha ambamo vipengele hivi vilitumika ikizingatiwa, inaweza kikisiwa kuwa waandishi hao wa awali wa riwaya za Kiswahili walilenga kuukuza msamiati wa Kiswahili, kwa kulitambulisha neno geni waliloliumia katika kazi hizo kando, na kulisisitiza.

2.3 Dhana ya riwaya ya Kiswahili ya kisasa.

Kulingana na Gromov (2014), ingawa riwaya ya Kiswahili ya kisasa inachukuliwa kuwa ibuko la kisasa, ni kazi iliyo na matini nyingi kuliko waandishi. Anawataja baadhi ya waandishi kama vile Kezilahabi, Mkangi na kazi zao. Anaendelea kusema kuwa kila mojawapo wa waandishi hawa kando na kuhusika pakubwa katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa, wamedhihirisha mchango mkubwa katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili kwa kuandika kazi nyingi za kifasihi, zinazorejelea vipera vyote vya fasihi andishi; riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi.

Gromov (keshatajwa) anasemankuwa riwaya ya Kiswahili ya kisasa au jinsi inavyojulikana kama riwaya ya kimajaribio iliibuka miaka ya tisini kufuatia chapisho la riwaya za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991), zilizotungwa na Kezilahabi. Hii ni dhihirisho kuwa riwaya hii iliibuka nchini Tanzania kabla ya Kenya. Mkangi anasemakana kuwa mwandishi wa kwanza wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa nchini Kenya kupitia kwa riwaya ya *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995).

Gromov anaelezea kuwa, riwaya ya Kiswahili ya kisasa inatofautiana na ile ya awali kimaudhui na kimfumo. Kulingana naye, riwaya za awali za Kiswahili za miaka ya sabini na themanini zilizoandikwa na waandishi kutoka Kenya na Tanzania zilijikita zaidi katika uhalisia wa kijamii, na ziliangazia zaidi changamoto ambazo nchi hizo zilikuwa zikikumbana nazo.

Gromov (keshatajwa) anasema kuwa riwaya ya Kiswahili ya kisasa katika urasmi wake wa kimitindo hutambulika kutokana na uhusiano wa karibu na maandishi ya baada-usasa, kwa kuzingatia mifumo ya kiparabola na ya ki - istiara kinathari. Gromov anaendelea kusema kuwa kimaudhui, shughuli kuu miongoni mwa waandishi wa riwaya hizi siyo tu maendeleo yanayotokea katika eneo la Afrika Mashariki bali pia uoga kuhusu siku zijazo za bara la Afrika na hatima ya binadamu kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Gromov, waandishi wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa wanaonelea kuwa bara la Afrika na raia wake wanatishiwa na maadui wakuu watatu ambao ni utandawazi, ukoloni mambo - leo na ubinafsi. Kulingana na Gromov, maadui hawa watatu polepole wamejipenyeza katika jamii na kuchangia katika usambaratishaji wa miundo - msingi ya jamii kwa kuutisha utu, mapenzi na kiini cha ubinadamu.

Gromov anasema kuwa kufuatia changamoto hizi zinalolikumba bara la Afrika, waandishi wengi wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa hushughulika na kazi inayozua taswira ya kitabiri na ya kidaistopia kuhusu ulimwengu – kabla na baada ya kusambaratika, uliyozama katika uongozi wa kiimla, unaokumbwa na njaa, uliozama katika mazingira yaliyoharibiwa na kiwango kikubwa cha umaskini kufuatia kuporwa kwa uchumi na viongozi.

Hata hivyo, kando na changamoto hizo, waandishi hawa wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa hujaribu kutoa suluhu kwa baadhi ya changamoto hizi, hususan jinsi binadamu anavyoweza kukombolewa na kuukomboa ulimwengu kwa ujumla. Kwa kufanya hivyo, waandishi hawa huwa wanawapa wasomaji tahadhariwa na pia huwapa matumaini.

Gromov (2014) anasema kuwa kutokana na masuala haya yanayomlenga Mwafrika barani, wengi wa waandishi hawa huwa na motifu inayowiana ya safari, miongoni mwa vigezo vingine vinavyokaribiana ambavyo hutumika katika uchaguzi wa riwaya hizi ili zitafitiwe.

Gromov anasema kuwa miongoni mwa riwaya za Kiswahili za kisasa ni pamoja na ;

Babu Alipofufuka (2001). Mohamed, S. A.

Dunia Yao (2006). Mohamed, S.A

Walenisi (1993). Mkangi, K.

Bina-Adamu (2002). Wamitila, K.W.

Musaleo (2005). Wamitila, K.W.

Mafamba (2008). Olali, T.

Watu wa Gehenna (2012.) Olali, T.

Upekuzi wa riwaya hizi kwa jicho la ndani unaonyesha kuwa zina uhusiano wa karibu sana. Mihimili mikuu inayodhihirika wazi ni maono ya baadaye ya waandishi, changamoto na suluhu na jinsi inavyoendelezwa na nguli. Waandishi hawa wanalidhihirisha bara la Afrika na ulimwengu mzima kama jamii ambayo polepole inasambaratishwa na majanga ambayo yameumbwa na binadamu. Binadamu wenyewe wanalaumiwa kwa kutochangia katika kuyasuluhisha majanga haya kwa kutotumia fikira na ujuzi walio nao.

Majanga haya yanautishia ulimwengu kupitia kuzoroteka kwa uchumi, mazingira, miundo - msingi, kukithiri kwa utabaka miongoni mwa dhuluma zingine. Nguli katika riwaya hizi wameonekana kuchangia pakubwa katika uhamasishaji wa wananchi na utekelezaji wa mapinduzi yanayochangia katika ukombozi kamili wa jamii.

Kwa mujibu wa Gromov (keshatajwa), riwaya hizi zinachukuliwa kama riwaya za Kiswahili za kisasa kufuatia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kuangazia changamoto zinazoyakumba mataifa mengi barani Afrika na jinsi majanga hayo yanavyoweza kusuluhishwa kupitia kwa mapinduzi, jambo ambalo riwaya za awali za Kiswahili ziliepukana nalo. Hii ni riwaya ambayo haijifichi katika maadili ya uongo, uoga, matumaini yasiyokuwepo bali inaielezea jamii kama ilivyo, huku ikijaribu kuipa jamii suluhu.

2.4 Kiishilio

Kwenye sura hii, dhana ya riwaya, riwaya ya kisasa na riwaya ya Kiswahili ya kisasa ilijadiliwa kwa undani huku ikibainika kuwa riwaya ya kisasa ya Kimagharibi na ya Kiswahili ya kisasa zinatofautiana katika vigezo mbalimbali kama vile vya umri, mazingira na maudhui. Aidha ilibainika kuwa riwaya ya Kiswahili ya kisasa inao mchango mkubwa wa kuchangia katika ukombozi wa jamii kwa ujumla.

SURA YA TATU: RIWAYA YA MKAMANDUME

3 Utangulizi

Sura hii iliishughulikia riwaya ya *Mkamandume* kwa kuihakiki kimuhtasari huku viakifishi kama mojawapo ya vipengele vya kigrafolojia vilivyotumiwa na mwandishi vikijadiliwa kwa undani. Aidha, iliweza kuangazia hatua mbalimbali ambazo ni mwafaka katika usomaji na uelewa wa kazi ya fasihi kwa minajili ya kuibuka na uhakiki uliyo bora.

3.1 Hatua za usomaji mwema

Wamitila (2008) anasema kuwa usomaji ni dhana muhimu katika uchambuzi wa kazi ya fasihi, na ni mfanyiko ambao unahusisha pande nyingi. Anaendelea kusema kuwa matini za kifasihi huwa hazijakamilika hadi zikamilishwe na wasomaji. Kulingana naye, uzoevu anaokuwa nao msomaji huathiri kwa kiwango kikubwa jinsi anavyoichanganua kazi ya kifasihi, hali ambayo hueleza kwa nini hadithi moja ikaweza kupata fasiri tofauti kutegemea wasomaji mbalimbali. Anatupa hatua mahususi ambazo mhakiki anahitaji kuzingatia ili kupata ujumbe uliyomo katika matini..

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), hatua ya kwanza anayoitaja ni usomaji. Anasema kuwa ni vyema ikiwa msomaji ataisoma kazi ya fasihi kwa zaidi ya mara moja ili aweze kuielewa kwa vile huo ndio msingi wa uhakiki. Hatua ya pili ni ufafanuzi. Anasema kuwa katika ufafanuzi, msomaji hupata maana ya kimsingi ambayo ndiyo maana kwa msomaji wa kawaida. Kwa kuwa mhakiki siye msomaji wa kawaida, analazimika kuipa kazi hiyo maana

ya ndani. Hatua ya tatu ni ile ambayo inahusu fasiri. Hii hushughulika na ile hali ya mhakiki kukifafanua kinachozungumziwa katika matini. Hatua inayofuatia ni ile ya uchambuzi na uchanganuzi.

Kulingana na Wamitila (keshatajwa), hatua ya uchambuzi na uchanganuzi inahusu kule kuviangalia visehemu mbalimbali na jinsi vinavyohusiana na kutenda kazi. Katika hatua hii, mhakiki huangalia muundo na athari zake, uchunguzi wa fani, tamathali za lugha miongoni mwa vipengele vingine. Suala la mjadala ni miongoni mwa hatua zinazopaswa kushughulikiwa na mhakiki. Hatua hii huongozwa na dhana ya kiulinganishi kwa kuangalia pande zote za ubora na udhaifu. Anataeleza kuwa hatua ya mwisho ni tathmini ya uamuzi. Hapa mchango wa kazi hiyo huangaziwa kwa kina kabla ya kufanya hukumu. Anasema kuwa hukumu bora hutokana na misingi mipana ya uhakiki.

Mawazo ya Wamitila yanashadidiana na ya Zhukovska (2010) ambaye ametoa vipengele vingine zaidi ambavyo ni vya muhimu katika uhakiki bora wa matini kifasihi. Kipengele cha kwanza anachokitaja ni wahusika. Kwa maoni ya Mohamed (keshatajwa), wahusika ni viumbe au vivuli vya mawazoni vinavyoumbwa na mwandishi na kuibuka katika kazi yake.

Anasema kuwa katika riwaya, vivuli hawa huishi katika simulizi na maelezo. Wamitila (keshatajwa) anasema kuwa mhusika ni akipatacho msomaji katika matini ya kifasihi anapojiuliza swali kuhusu “mtu” au “mtendaji”. Anaendelea kutueleza kuwa wahusika wa fasihi hudhibitiwa pakubwa na majukumu ya kiuajumi katika kazi za fasihi husika.


Mwananaratolojia maarufu Bal (1985) anataja mbinu mahususi za kumtambua mhusika. Anasema kwamba, ni vyema kuuchunguza urudiaji wa sifa zilizotajwa kuhusu mhusika huyo katika kazi ya fasihi. Pili anasema kuwa ni ukusanyaji wa ujalizaji wa sifa ambazo zinasaidia kuelezea wasifu fulani. Tatu anataja uhusiano wa mhusika mmoja na wahusika wengine. Nne anasema kuwa ni muhimu kuchunguza mageuko ya mhusika huyo na kiasi cha mageuko hayo. Kwa mujibu wa Zhukovska, mhusika muhimu katika kazi hii ni nguli ambaye hujengwa na mwandishi hadi akakamilika. Hata hivyo, anasema kuwa usimulizi huo haukamiliki bila nguli kukumbana na mkinzani.

Kipengele cha pili anachokitaja ni uhusika. Mohamed (keshatajwa) anasema kuwa uhusika hauwezi kukamilika pasipo na ushuba. Anasema kuwa ushuba huo umo katika kijielezi wapi na lini? au mazingira ya ukumbi ambamo mhusika huibukia. Wazo kuu linaloibuka hapa ni kwamba mazingira na msingi wa mhusika uangaziwe vyema li mchango wake uweze kujitokeza wazi. Zhukovska (keshatajwa) anasema kwamba kuna aina mbili ya uhusika. Uhusika wa moja kwa moja ambao msimulizi au mwandishi anamwelezea kwa ufupi msomaji kuhusu jinsi mhusika alivyo, ilihali katika uhusika usiyo wa moja kwa moja, mwandishi anaonyesha jinsi mhusika alivyo, kupitia kwa maneno anayotoa kuhusu mhusika mwenzake, mavazi yake, fikira, sura yake na hata matendo.

Kipengele cha tatu ni mandhari. Kwa mujibu wake, mandhari ya usimulizi hushughulika na muda na mahala ambapo usimulizi unatukia. Pia anataja msuko kama kipengele kingine katika uchambuzi wa matini. Wamitila (2008) anafafanua msuko kama mfuatano wa matukio katika kazi ya fasihi bila kuzingatia mpangilio wa kiwakati. Anasema kuwa ni vyema msomaji anapoanza kuisoma kazi ya kifasihi awe na hamu ya kuivumbua hadithi hiyo kwa kujiuliza swali la nini kilichotokea.

Zhukovska (keshatajwa) anasema kuwa msuko ni mfululizo wa matukio na mchango wa wahusika, maudhui na ujumbe unaojitokeza kutokana na matukio hayo. Anaendelea kusema kuwa msuko hufululiza kupitia kwa mgogoro kati ya mhusika mkuu na wapinzani wake kama inavyojitikeza katika haram ya G. Freytag iliyochoywa hapa.

Piramidi / Haram ya Freytag



1-Piramidi /Haram ya Freytag

Zhukovska (keshatajwa) anaelezea kuwa kupitia kwa mwanzo wa mgogoro, msomaji anahitaji kupata habari za kimsingi kuhusu hadithi; wahusika, mandhari pamoja na historia fupi kuhusu hadithi. Visa kadha hutokea katika sehemu ya mwanzo mwa mgogoro ambavyo huenda vikaeneza mgogoro huo. Sehemu ya kilele huashiria kiwango cha juu zaidi cha mgogoro, na hapo mhusika mkuu anawajibika kuchukua hatua fulani ambayo itamuathiri vibaya au itampa nafuu katika hadithi.

Sehemu inayofuata kilele huathirika na kushuka kwa matukio, kisha matokeo hufikiwa. Kulingana naye, hadithi yenye msuko wa aina hii huwa imekamilika na husemekana kuwa na mfumo wenye msuko funge. Ile hadithi ambayo haizingatii viwango hivi katika msuko wake huchukuliwa kuwa na msuko ulio wazi kinfumo. Wamitila (keshatajwa) anasema kuwa misuko ya kazi ya fasihi huwa msingi wa burudani muhimu katika usomaji - burudani ya kutokamilika.

Katika riwaya teule, mwandishi anatupa msingi wa mhusika Mkamandume na jinsi anavyojibidiisha kimaisha kwa kushughulika na ukulima wa aina mbalimbali ya mimea. Bidii yake miongoni mwa mwenzake inamfanya kufikiriwa kama mkulima bora katika eneo la Malelejimema. Hata hivyo, bidii yake haimnufaishi na anapoikosa tuzo ya mkulima bora, anakata tamaa, anachukua hatua ya kuifyeka mimea yake yote.

Mkamandume amegundua kuwa adui wake na wa jamii nzima ni Mtemi na vibaraka wake. Basi anaamua kuchukua hatua ya kubuni mikakati ya kumwondoa Mtemi. Anatekeleza maangamizi ya Mtemi na matokeo yanakuwa kuangamizwa kwa Mkamandume na askari wa Mtemi. Hata hivyo, jamii mpya inazaliwa.

Kipengele kinachofuatia ni mfumo na mbinu za usimulizi, mbinu za kimtindo, toni na maudhui kama vipengele muhimu katika uhakiki wa riwaya kimtindo. Anasema kuwa usimulizi ni hadithi ya msimulizi kuhusu matukio na hatua za wahusika kuhusu matukio hayo. Wamitila anasema kuwa usomaji ni lazima ubainishe mitazamo inayopatikana katika kazi ya kifasihi. Kulingana naye, kuna mitazamo kadha katika upambanuzi wa kazi za kifasihi na anataja nafsi ya kwanza, nafsi ya tatu na mitazamo changamano.

Kufuatia utaratibu huu wa usomaji bora, msomaji anapata ujuzi wa kuisoma na kuihakiki kazi ya fasihi bila kukumbana na changamoto zozote.

3.2 Uchanganuzi wa matini (Riwaya ya Mkamandume)

Riwaya ya *Mkamandume* ni utunzi wa Said A. Mohamed ambaye ni profesa mtajika katika taaluma ya Kiswahili kote ulimwenguni. Alizaliwa kisiwani Pemba mwaka wa 1947 na akayapokea masomo yake katika taasisi mbalimbali za kielimu kisiwani humo na pia ughaibuni. Amewahi kuhudumu katika nyadhifa mbalimbali barani Afrika na ng'ambo, na kwa sasa amestaafu na anaendelea kuihudumia jamii kwa njia mbalimbali.

Said A. Mohamed kwa hakika ni mtalaamu katika ulingo wa fasihi ya Kiswahili na umaarufu wake, kama alivyosema Gromov (2014)), umechangia pakubwa katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Kufikia sasa amekiri kuviandika vitabu zaidi ya hamsini na tano, vinavyorejelea vipera vyote vya fasihi andishi.

Kama ilivyo kawaida kwa mwandishi kuathiriwa na mazingira anamozaliwa na kukulia, Said A. Mohamed amedhihirisha athari hizo katika kazi yake. Ameipa riwaya hii jina la *Mkamandume*, na kufuatia utafiti wetu, imebainika wazi kuwa jina hili linayarejelea yale magofu yaliyosalia katika kijiji cha Pujini kisiwani Pemba alikozaliwa mwandishi. Magofu haya yanahusishwa na utawala wa kiimla wa Wareno, na yamewahi kutumiwa kama gereza. Taasisi hizi za magereza zinatumiwa kuwatenganisha watu na utu (jamii). Hata hivyo, Hii ni ishara kwamba mwandishi hajayasahau mazingira alimozaliwa.

Mkamandume ni riwaya iliyochapishwa mwaka wa 2013 na shirika la uchapishaji la Longhorn. Katika tabaruku ya riwaya hii, mwandishi anatujuza kuhusu wahusika waliozama usingizini usiku na mchana na walalao bila chakula ambayo ni ishara ya ukosefu wa miundomsingi miema. Kwenye tanbihi ya riwaya, mwandishi amekiri kuwa hii riwaya kwa hakika ilimchukua muda mrefu mno na anakisia kuwa huenda ikawa hata zaidi ya miaka ishirini. Kwa hakika, muda huo wa uandishi ni dhihirisho kamili kwamba mwandishi alikuwa akiitazama jamii rejelewa kwa jicho pekuzi.

Kwenye wimbo wa Jauhar, tunafahamishwa kuwa mazingira ambamo wananchi wanaorejelewa riwayani wanaishi ni kama yale ya kibahari. Bahari kwa kawaida humiliki vitu vingi ambavyo vyaweza kuwa wanyama wakubwa wakubwa na wadogo wadogo kimofolojia. Ni nadra sana papa kumuomba ruhusa kidagaa ili anywe maji na katika zile harakati zake kunywa maji, huenda kwa bahati mbaya akamumeza kidagaa katika mazingira ya hali hii. Wanajamii wengi wanaangamia licha ya ujuzi na tajriba waliyonaao kuhusu kuishi kwao kwenya mazingira haya. Dhamira ya kisa hiki ni kwamba hao ni wanajamii ambao wanahitaji kukombolewa dhidi ya dhuluma inayoendelezwa na viongozi wao.

Riwaya hii ina kurasa mia tano ambazo zimegawika katika sura hamsini na nane. Sura ya kwanza ndiyo fupi zaidi riwayani na imejumulishwa katika ukurasa mmoja wenye maneno mia moja themanini na tano, ilihali sura ya arobaini na moja ndiyo ndefu zaidi na kurasa ishirini na mbili. Inasadifu kuwa mhusika mkuu riwayani amepewa jina la Mkamandume, mhusika anazungumza na nafsi yake.

Mwandishi anatupa taswira ya Wanamalelejimema, jamii ya watu wanaoishi bila chakula kwa sababu ya mifumo miovu ya uongozi. Mkamandume ndiye nguli katika riwaya hii. Mhusika huyu amechorwa kama mwenye kiwango cha juu cha uvumilivu; aliyavumilia madhila na haramu za *'boss'* wake kwa muda mrefu na hii ilidhihirika kupitia kwa matukio mengi yakiwemo siku ya kumtuza mfanyikazi bora.

Wengi walimfahamu Mkamandume kama mfano mwema wa wafanyikazi, aliyestahili tuzo. Uongozi mbaya unadhihirika wakati *boss* wake badala ya kumtuza Mkamandume, anamtuza Zuhura Saleh Mcheshi, msichana aliye na uhusiano wa karibu na *Boss*. Jina la Zuhura Saleh Mcheshi linapotajwa na *Boss* kama mfanyakazi bora kutokana na upendeleo, wafanyakazi wote wanastaajabu kama inavyonukuliwa hapa; “ *Zawadi ya mfanyakazi bora mwaka huu,*” *alirudia boss kwa msisitizo,*

“ *inakwenda kwa Zuhura Saleh Mcheshi.*” *Kofi ziliuma!*

Kejeli kaning'inia hewani....uk.27.

Hata hivyo, tunaelezwa kuwa lilikuwa jambo la kawaida kwa zawadi hiyo kumwendea mhusika asiyestahili.

Mambo kadhaa yanajitokeza katika muktadha huu. La kwanza ni kwamba bidii aliyokuwa nayo Mkamandume ilididimia kutokana na kutotuzwa kama mkulima bora. Mkamandume aliweza kukipoteza kile kitita cha shilingi laki tano alizopewa mkulima bora ambazo zingemwauni vyema maishani. Imani na heshima waliyokuwa nayo wafanyakazi kwa Mkamandume pia ilipotea. Zuhura anapewa zawadi hiyo kwa vile anapendelewa na *boss*.

Mkinzani wa Mkamandume katika hali hii ni yule *boss* Mtemi mwenye upendeleo. *Boss* anayerejelewa riwayani humu amesababishia jamii umasikini kutokana na sera mbaya za uongozi, kiwango kwamba Mkamandume amekosa hata mahitaji yake ya kimsingi. Mkamandume anaeleza jinsi ukulima ulivyopoteza thamani miongoni mwa wanajamii wote ndiposa anaamua kuifyeka mimea yake ya mihogo na migomba kwa hasira,

kudhihirisha hali hiyo. Hawezi kumudu mavazi mema. Mparapata wake unaostahili kumwezesha kusafiri kwa haraka umekuwa hafifu na ni mzigo mkubwa kwake. Analazimika kwenda kukopa pesa kutoka kwa adui yake. Mambo haya yanamfanya awe na maumivu ya ndani kwa ndani yanayompekecha kila uchao.

Wakaazi wa Malelejimema wengi kama vile Soud wanalazimika kukimbilia nchi zingine, zenye uongozi mwema huku Mkamandume akidhihirisha kiwango cha juu cha uzalendo. Wananchi wengi wa Malelejimema wanakuwa masugu. Wengine kama vile Viwe anatoka likizo ya kukilea kitoto chake na anakuta kazi yake ikiwa imenyakuliwa na mwingine. Hakati tamaa na bidii aliyo nayo Viwe inamwezesha kujiunga na taasisi za elimu ambako anafaulu kujiendeleza kimasomo. Soud anarejea na wanashikana na Viwe katika harakati za kuwahamasisha wanajamii kuhusu uongozi.

Muungano huo wa wanamapinduzi unawajumulisha wengi, wake kwa waume, wazee kwa vijana wakiwemo Nadia, Mzee Sleyyum, Mkamandume, Viwe na Soud. Wasiwasi imetanda kote miongoni mwa wanajamii kiasi kwamba raia sasa hawaaminiani. Sasa wanaazimia kuyashughulikia mambo makubwa makubwa yatakayowapa ukombozi wa mwisho. Cha ajabu ni kwamba, matukio haya hayajafungwa tu katika hizi jamii za Msera na Malelejimema bali mwandishi anatueleza kuwa yanajitokeza pia Umarekani na Japani.

Kilele cha ukombozi katika jamii hii kinatukia kupitia kwa maandamano ambako Mkamandume na wenzake walishiriki na lengo la kutekeleza mapinduzi ya kumuondoa

hasidi Mtemi au kwa jina la utani *Boss*. Mwandishi anamrejelea Mkamandume na jinsi anavyochangia katika mapambano ya ukombozi, huku akitumainia kuwa maisha yataimarika.

Mkamandume kwa hivyo anaufikia uamuzi wa kumkama ndume; kufanya lisilotarajiwa kwa kumwondoa Mtemi na vibaraka wake uongozini na duniani kote. Anayaendeleza mapinduzi hayo kwa kubuni mikakati ya kuwangamiza hawa mahasidi. Anajificha chini ya Mlangilangi akifahamu kuwa Bwana Shombo mojawapo wa vibaraka wa Mtemi atapita pale. Anamwangamiza Shombo kwa shambulizi moja la upanga unaoking'oa kichwa cha mhusika huyu. Baada ya shambulizi hilo, maandamano yanachacha huku wengi wakishiriki. Bwana Sleyyum anatoa mabasi yake kwa ajili ya kuwasafirisha wapiga ngoma za ki- Malelejimema ili kuwahamasisha watu kuhusu maandamano hayo.

Mkamandume anautumia ujuzi na tajriba yake tena kumwangamiza Mtemi kwa kumfyeka shingo, kisha anajumuika na waandamanaji ambao wanadhihirisha umoja wa kiwango cha juu. Hatimaye, Mkamandume anauawa na polisi wa *valantia* kwa kupigwa risasi. Vua zito linanyesha usiku na mchana baada ya kuuawa kwa Mkamandume ambalo linalenga kuuosha uchafu uliyokuwa umeenezwa na uongozi dhalimu wa Mtemi.

Siku ya kuzikwa, Mkamandume anasemekana aliipasua sanda aliyofungwa nayo na kuwapungia buriani ya mwisho waliokuja kumzika kudhihirisha kuwa hakufa bali kavuka daraja nyingine ya maisha. Wanawe Mkamandume walioshiriki katika mapinduzi Viwe, Nadia na Soud wanasemekana kumezwa na wazee wa kijiji cha Msera ili wawalinde dhidi ya

hila za polisi waliowasaka kwa ghamu. Wanamalelejemema na jamii ya Msera kwa ujumla waliweza kuzaliwa upya na kuishi maisha mema baadaye.

3.3 Viakifishi na jinsi vilivyotumika katika ujenzi wa riwaya ya *Mkamandume*.

Chukwu (2010) anasema kuwa viakifishi ni alama za kuonwa ambazo hutumika kimaandishi kwa njia ya kifasaha katika mfuatano uliyokubalika. Anaendelea kusema kuwa alama hizi huzingatia kanuni zilizokubalika kuhusu matumizi na dhima yazo kiisimu, ingawa mwandishi huweza kuzitumia visivyo ili kuwasilisha ujumbe wake, na katika kufanya hivyo, alama hizi huzingatia upeke wa mwandishi kimtindo.

Riwaya ya *Mkamandume* imejengeka kwa vipengele vingi. Mwandishi wa riwaya hii alivitumia viakifishi mbalimbali ambavyo vilijadiliwa kiundani ili kutafakari ujumbe uliolengwa. Miongoni mwa viakifishi hivyo ni pamoja na ving'ong'o, vistariungio, alama za kunukuu, vinyota, udondoshaji, vihisishi, deshi, viulizi, mabano, koma, koloni, semi-koloni, vikomo. Viakifishi hivi vilishughulikiwa kwa msingi wa Chukwu (keshatajwa) ambaye aliviainisha viakifishi kwa makundi matatu ambayo ni; viakifishi vya neno, vya ndani na vya tamati.

3.3.1 Viakifishi vya neno

Kulingana Chukwu, hivi ni viakifishi ambavyo hupachikwa katika neno na hujumlisha ving'ong'o, kistariungio, alama za kunukuu na vinyota. Anasema kuwa ni viakifishi ambavyo vitajitokeza katika neno bila kuhitilafiana na neno hilo. Kila kiakifishi cha neno kilishughulikiwa kwa mapana huku mifano mwafaka ikiangaziwa jinsi viakifishi hivi vilivyotumika katika riwaya teule.

3.3.1.1 Ving'ongo (')

Kisarufi, ving'ong'o huwakilishwa na alama zilizo katika mabano. Chukwu amevielezea ving'ong'o kama viakifishi vya ndani kwa vile vinapachikwa katika neno. Anasema kuwa kando na kuendeleza sauti ya ung'ong'o miongoni mwa maneno yanayojulikana waziwazi, ving'ong'o hutumika kuendeleza dhana ya ufupishaji au udondoshaji.

Katika riwaya ya *Mkamandume*, ving'ong'o vinajitokeza mwanzoni mwa riwaya katika sehemu ya tabaruku hadi mwishoni mwa utanzu. Vimetumika katika maneno mbalimbali kama vile N'najua, mi'n'na (uk iii), kinying'inya (uk. 1), 'kujisibabi, n'takueleza (uk 2), nd'o 'ivyo (uk. 10), kung'ang'ania (uk.21), baba'ake (uk.23), kumong'onyoa (uk.33), kumng'oa,(uk.36) linaning'inia(uk.23), kulimung'uya, mama'ke, ng'o, n'toke, ng'ambo, n'na, ak'enda, n'kuvute, tu'sende, maka'zi, 'ye, 'mi, us'o, waona'ni, aking'ong'ona miongoni mwa mengine mengi.

Katika maneno haya, mwandishi amedhihirisha kwamba kuna viambajengo vya maneno ambavyo amevichuna. Huu ni mtindo mpya wa uandishi katika riwaya, ingawa ni wa jadi katika utanzu wa ushairi kwa vile hutumika na washairi na lengo la kusawazisha mizani katika mishororo. Katika riwaya hii, matumizi ya ving'ong'o yamelenga kuipa lugha sura ya kimazungumzo kama washairi wanavyofanya huku matamshi yakiendeleza hisia za wasemaji.

Kwa mujibu wa Wamitila (keshatajwa), uakifishaji wa aina hii unahusika na mitindo ya kisimulizi ya kazi hasa riwaya za kisasa na hulenga kuichimuza kazi hiyo. Kando na matumizi hayo jinsi anavyoelezea Wamitila, tunaweza kukisia kwamba ving'ong'o vinapotumika katika uandishi wa aina hii, vinazua suala la uchumi katika lugha kwa vile idadi ya viambajengo vya lugha hupunguzwa. Kuna uwezekano riwaya hii ingekuwa ndefu zaidi ikiwa haingetawaliwa na ving'ongo, kuashiria kudondolewa kwa vipashio vingine vya lugha. Kwa hivyo riwaya ya *Mkamandume* imejengeka kwa alama za ving'ong'o.

Kipacha (2003) ameishughulikia lahaja ya Kipemba na amesainisha leksimu za lahaja hii ambazo zinadhihirisha wazi matumizi ya alama ya ving'ong'o katika udondoshaji wa maneno. Hii inajitokeza kwa maneno kama vile s'emeji badala ya shemeji, s'ingo badala ya shingo miongoni mwa mengine, kando na utokeaji wa mofimu tofauti kama vile i'gori badala ya kigoli.

Katika sentensi kama vile Viwe ak'enda moja kwa moja mpaka akasimama pua na mdomo na babake inayopatikana katika ukurasa wa 466, nafasi ya sauti [a] imechukuliwa na king'ong'o na mifano hii inadhihirisha wazi kuwa huenda mwandishi wa riwaya teule aliathirika na lahaja ya Kipemba, na hivyo basi kuiendeleza athari hiyo katika kazi yake. Alama hii inapotumika katika muktadha huo inaimarisha uchimuzi.

3.3.1.2 Kistariungio (-)

Crystal (keshatajwa) anasema kwamba kiakifishi hiki pia kinajulikana kama kistari kifupi na hudhihirisha kufungamanishwa kwa sehemu za neno. Anaendelea kusema kuwa alama hii huwa na matumizi yafuatayo kwa ujumla:

- i. Inatumika katika usilabishaji. Katika hali hii, kistariungio huunganisha silabi zilizotenganishwa kwa mfano, ka-la-mu.
- ii. Alama hii pia hutumika kuunganisha maneno mawili au matatu ambayo huwa na maana moja kwa mfano Mbwa-koko aliuma mwana-haramu. Nawatuma kama wana-kondoo miongoni mwa mbwa-mwitu.
- iii. Inatumika kutambulisha mofu funge miongoni mwa maneno ambayo fasiri ya maneno hayo huleta utata kimaandishi, hususan katika lugha ya Kiingereza.
- iv. Inatumika katika lugha ya Kiingereza kuunganisha vipengele viwili wakati ambapo herufi za mwisho (ziwe konsonanti au vokali) za kipengele cha kwanza ni sawa na herufi ya kwanza ya kipengele cha pili.

- v. Inatumika kuunganisha viambishi awali vya maneno ambayo viambishi awali vya maneno hayo huwa yameanza kwa herufi kubwa katika lugha ya Kiingereza kwa mfano, *'Anti-Semitism, Pro- American, Un-English'*.
- vi. Inatumika kuunganisha maneno ya Kiingereza ambayo hutanguliwa na kiambishi *'ill'* na *'well'* kwa mfano: *'ill-formed (ness), ill-mannered, well-behaved'*
- vii. Inatumika kuonyesha sehemu ya idadi kamili katika lugha ya Kiingereza kwa mfano *a two-third majority, one-tenth.*
- viii. Inatumika kurejelea au kuonyesha tarehe kwa mfano watu wengi walikufa tarehe 07-08-1998.

Alama hii imetumika katika ujenzi wa riwaya teule kupitia kwa maneno kama vile; yanasonga mbele - lazima yasonge (uk.1), Mungu- mdogo (uk.5), vikazaliwa pamoja - pacha, suala linabaki - usuli wako ni upi, ndio kileo - na kesho, ki – Katija (uk.16), kwa hakika imebaki fremu tu - fremu, si ndivyo ulivyoni amrisha nifanye-sasa, wamemgeukia Mkamandume - wengine kwa huzuni na wengine kwa inda, fedha bila ya shaka alizitaka - hasa kwa lile shimo, ki - Angela Davies (uk.44), ubavunu pake kalala Bi. Fuu - bibi yo mzaa baba, na kilipoingia tena, alitoa tena na tena - hivyo mpaka leo, ndio - kileo, Mungu - mdogo, mwanzo - mwanzo kabisa, ujiuji - kama tambarare - moto, katika upeo wa umri - miaka na mikaka - tekenyoza mikono, simulizi ya mbabe - simulizi aliyoiita jadi na usuli, hakumbakisha babake - kimo, miongoni mwa maneno mengine mengi.

Kutokana na matumizi ya kistariungio katika riwaya hii, inajitokeza wazi kwamba kiakifishi hiki kilitumika na lengo la kusisitiza ujumbe alioulenga kuupitisha mwandishi, kando na kuzua hisia nzito kuhusu mawazo yaliyopitishwa. Pia imetumika kuunganishia kiambishi ‘ki katika majina ili kuendeleza na kuelezea wanajamii duni, uduni uliotokana na uongozi mbaya.

3.3.1.3 Alama za kunukuu (‘ ’) (“ ”)

Crystal anasema kuwa alama hizi zaweza kujitokeza kama moja moja au mbilimbili kutegemea anayezitumia lakini anasema kuwa zote hutumika na dhima moja. Anaendelea kusema kwamba zinapotumika katika hali yoyote ile, huwa zinadhihirisha kuwa usemi huo ni ule uliotoka kinywani mwa mzungumzaji, ni usemi halisi. Kwa hivyo alama hizi hutumika kunukuu usemi halisi. Anaendelea kutueleza kuwa kando na matumizi hayo, vipengele hivi hutumika kunukuu anwani za vitabu, mashairi, nyimbo na majarida.

Kwa mujibu wa Crystal (keshatajwa), inatumika kutaja nukuu zingine katika matini. Alama hizi zimetumika sana katika riwaya na hivyo basi kuipa kazi hii uhai fulani hasa tunaposhuhudia Mkamandume akizungumza na wahusika wengine kama vile Nadia, Time na hata anapozungumza na nafsi yake. Mifano hii inadhihirisha jinsi mwandishi alivyokitumia kiakifishi hiki; “Sikiliza Mkamandume...” “Mkamandume hebu nikuulize...” (uk.1) “Mimi nakusimulia wewe...”(uk.4) “Geuka Mkamandume...”(uk.5) “Aaaaa” “*Bull shit*” (uk.86).

Kama wasemavyo Leech na Short (1981) kwamba dhana ya kimtindo ni kuwasiliana, kiakifishi hiki kando na kutekeleza majukumu ya kiisimu, kinaichimuza kazi hii kwa kumfikirisha msomaji

3.3.1.4 Vinyota (*)**

Aidha vinyota ni miongoni mwa viakifishi vya ndani ambavyo Chukwu (2010) alivishughulikia. Kulingana na Chukwu (keshatajwa), vinyota huwakilishwa na alama za vinyota vitatu. Anasema kuwa vinyota vinatumika kimatini kutekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo yafuatayo;

- i. Kuonyesha neno ambalo litaelezwa zaidi chini ya ukurasa. Kwa mfano, alipopata nafasi ya kuingia shule ya upili ya Starehe*, mwanafunzi huyo alijawa na furaha tele. *Starehe ni mojawapo ya shule zinazotoa matokeo mema nchini Kenya.
- ii. Kuleta usafidi kwa kuficha herufi au silabi katika neno ili kupunguza ukali wa maneno yasiyo na nidhamu au ya kuudhi yakitamkwa waziwazi kwa mfano, Rais aliwaita wananchi m**i ya kuku. Katika mfano huu, vinyota hivi vimetumika kuficha herufi [af] na ikiwa herufi hizi zingejumulishwa katika neno hili, lingekuwa ‘mafi’, ambalo ni neno lisilokuwa na nidhamu, likitumiwa katika hali ya kawaida na mtu wa kiwango au cheo cha Rais.

Mwandishi Said, A. Mohamed wa riwaya hii alivitumia vinyota kwanza katika tabaruku. Hata hivyo hakukitumia katika maneno bali katika utangulizi wa baadhi ya aya katika riwaya. Uchunguzi wa jinsi mwandishi alivyokitumia kiakifishi hiki unadhihirisha kuwa

alilenga kuisitiza ujumbe muhimu katika aya mbalimbali hivyo basi kuchimuza mawazo ya msomaji ili amakinikie sehemu hizo.

3.3.2 Viakifishi vya ndani

Kulingana na Chuku (2010), viakifishi vya ndani hujumlisha kipumuo (,) koloni au nukta mbili (:), nukta kituo au semi koloni (;), parandesi (), udondoshaji (...) kareti (^) na deshi (—)

Okunoye (2003) anasema kuwa viakifishi vya kati pia vinaitwa viakifishi vya maneno na vinatumika kudhihirisha kukatizwa kwa mfululizo wa mawazo kinasaba katika sentensi. Katika hali hii, ile kasi ya kusoma hupunguzwa wakati viakifishi vya kati vinapotumika ili kumwezesha msomaji kushika mawazo mapya, yanayoongezwa au kuondolewa katika matini na lengo la kumwezesha msomaji huyo kupata mkondo mpya ambao maandishi yamechukua. Katika kufanya hivyo, msomaji huweza kuibuka na ufasiri aliyolenga mwandishi.

3.3.2.1 Kituo, Koma au Kipumuo (,)

Chukwu (2010) anasema kuwa alama hii hutumika kuonyesha pumziko fupi katika sentensi, na pia kutenganisha viambajengo vya sentensi. Hata hivyo, Solomon na mwenzake (2009) wanaeleza kuwa alama hii inaweza kuwa na matumizi mengine mengi yakiwemo yafuatayo;

a) Kutenganisha maneno katika orodha kwa mfano;

i) Kudai mapenzi ni haki yake Time, kwa hivyo alikuwa tayari kumkabili tena Soud, mama'ke au hata baba'ke mripuo moto usiozimika (uk.40).

ii) Mtemi alikuwa kava bulbu! Suti: koti, kinusukoti, tai, suruali na viatu vya buti (uk.25).

b) Kutenganisha kirai au mawazo katika sentensi ikiwa kirai kielezi kinatangulia kirai kikuu, kwa mfano;

i) Kwa vyovyote vile, kila mtu siku hizi hubeba msalaba wake (uk.7).

c) Kutenganisha kirai kishirikishi kutoka kwa kirai kikuu ikiwa kuna mabadiliko katika mada kuu, kwa mfano;

i) Mkamandume alianza kuhisi upepo ukimvaa na kumparamia, yeye na mparapata wake (uk.3). (mabadiliko katika mada).

d) Kufungamanisha virai visivyo na masharti, ambavyo vinaweza kuwa na masharti, na hivyo basi kuifanya sentensi yote kuibua maana mpya, kwa mfano;

i) Punde baadaye mimea na miti ikachipua, na ilipochipua ikakua, na hatimaye ikakuza machaka na misitu na rutuba ya nchi ikatapakaa na kuenea (uk.12) (haina masharti).

- e) Kudhihirisha usemi halisi. Huu ni usemi ambao huwa jinsi ulivyotoka katika kinywa cha mzungumzaji, kwa mfano, “Baba, ‘uyoo, baba,” ki-Katija huku kikimfukuzia baba’ake kama kawaida yake kinapomwona akichomoza na mparapata wake (uk.13).
- f) Kudhihirisha matumizi ya kauli ya mneni ambayo huwa na dhima mbili. Dhima ya kwanza ni kumtambulisha mpokezi wa mazungumzo na kushika makini yake, na ile ya pili ni kuitambulisha mielekeo ya mzungumzaji kwa mzungumziwa (bila kuzingatia ikiwa mielekeo hiyo ni ya kiheshima, kirafiki au hata ya kinaya). Kauli za mneni kwa hivyo hudhihirisha uhusiano uliopo kati ya mzungumzaji na mpokezi wa mazungumzo hayo. Kauli za mneni hujitokeza mwanzoni, kati na mwishoni mwa sentensi.
- g) Kutambulisha maneno katika kirai, katika kijalizo au mrejeosawa, kwa mfano; Pale Msera, wakati huu, *tasnifa* iliyozea kumjia mara nyingi siku hizi, ilimjia tena Mkamandume.

Waldhorn na Zeiger (1980) wanaelezea kuwa matumizi mengine ya kipumuo ni pamoja na;

- h) Kuleta utata katika makala, kwa mfano katika kifungu hiki; Siku zile, walipofika hapo, yeye pamoja na babake, na majira yaliposadifu kuwa ya ukulima wa mpunga, na baada ya kula chochote walichochukua, waliketi kibandani kutazama konde waliyokwisha *iburuga*, au bahari ya mpunga uliokuwa ukitibua mawimbi ya kijani katika mtekenyo wa upepo huku ndege wakicharukwa kudowea kulikwepa jicho la mwanadamu lililokuwa wazi huku mwanadamu mwenyewe akibwata “We, we, we...shiii...uyooooo, haya, haya, haya, haya...toka...toka...toka...ooooo...kimbia ...shiii...” uk. 35.

Hiki kifungu kinaweza kupewa fasiri mbalimbali na hivyo basi kuzua utata. Alama hii pia inatumika kutenganisha mwaka na mwezi katika kuangazia tarehe au sherehe muhimu kwa mfano; i) Mei, 27, 2006, ii) Krismasi ya,2016

- i) Kipumuo hutumika kutenganisha sehemu za majina ya Kijiografia na anwani kwa mfano,
- ii) Magofu ya Mkamandume, kisiwani Pemba.
- iii) Inatumika baada ya maamkuzi na dibaji katika uandishi wa barua, kwa mfano; Kwa mpenzi, na Wako mwaminifu,.
- iv) Inatumika katika tarakimu kugawa kwa mafungu ya elfu, kwa mfano Mkamandume alikwisha ipangia mangapi zawadi ya 500,000 shilingi kwa tama kuwa yeye ndiye angelikuwa mshindi (uk. 28).
- v) Inatumika kutenganisha maneno yanayokinzana katika sentensi kwa mfano Licha ya jasho, kamiminika hata matone ya damu yake. uk. 29.

Hata hivyo, wataalamu hawa wanaweka masharti ambamo ikiwa kipumuo kitatumika tofauti, basi kitadhihirisha ukiukaji wa kaida za kiisimu. Wanasema kuwa kipumuo kisitumike kutenganisha kishazi kutoka kwa kitenzi. Pia wanasema kuwa kipumuo kisitumike kutenganisha kitenzi kutoka kwa tukio na pia kisitumike kutenganisha kijalizo kutoka kwa kitenzi kiunganishi. Wanasisitiza kuwa kisitumike kutanguliza au kufuata kitajwa au kijisehemu cha kwanza katika mfululizo wa vitu vinavyotajwa.

Kipumuo kimeangaziwa katika miktadha miwili. Muktradha wa kawaida ndiyo ule wa kiisimu. Katika ule muktradha wa kimatini, kiakifishi hiki kimetumika kwa mapana katika kuimarisha uchimuzi riwayani.

3.3.2.2 *Koloni* (:)

Watalaamu Waldhorn na Zeiger (1980) wanasema kuwa alama hii hutumika katika maandishi kudhihirisha kuwepo kwa taarifa au maelezo au ufafanuzi zaidi unaofuatia kifungu kilichotangulia. Ni alama inayodhihirisha matarajio fulani. Ezugu na wenzake (keshatajwa) wanakubaliana kuwa koloni ni alama ambayo inamtambulisha na kumtahadharisha msomaji kuhusu chochote kitakachofuatia katika maandishi. Anaainisha matumizi yafuatayo ya koloni kimaandishi kw ujumla:

- i) Inatumika kutenganisha taarifa mbili, ambapo ile ya pili inaifafanua ile ya kwanza. Katika hali hii, ile taarifa inayotofautishwa huwa ni kirai, lakini kile kirai cha pili hukinzana au hukifafanua kile cha kwanza. Koloni katika muktradha huu hutumika kumaanisha “kwa hivyo”. Mifano ifuatayo kutoka riwayani inadhihirisha matumizi ya kiakifishi hiki: Wimbo wa ‘Jauhar’: kikundi maarufu cha taarab cha Mombasa. ‘ Mkamandume: mguu juu, mguu chini, akasukuma *pedeli*. Mtekenyeko ulipopoa, mandhari ikawa pande tupu: tepetepe; nyekenyeke, ujuuji – kama tambarare – moto lililotibuliwa na volcano (uk.iv).’
- ii) Hutumika kutenganisha sentensi mbili tofauti, ambapo ile ya pili huelezea sababu za kuwepo kwa ile ya kwanza. Katika hali hii, koloni inachukua nafasi ya ‘kwa sababu’

kwa mfano; Ndipo tena kila kitu kikawa kibichi: ushupavu wa Time, utundu wake, upevu wa mawazo yake, ujaji wake, uzuri wake – vyote vilikuwa vibichi! (uk. 84.)

iii) Hutumika kutaja bidhaa mbalimbali katika orodha. Katika hali hii, koloni inatumika kama ‘yani’ kwa mfano; Time akabaki kusumbuka kwa kila jambo: fikra pomoni, wasiwasi wa nyuma na mbele, na hasa mbele anakokwenda lakini asikojua (uk.91).

iv) Hutumika kutanguliza nukuu rasmi au nukuu refu, kwa mfano ;

“ Zawadi ya mfanyakazi bora mwaka huu : inakwenda kwa mchapakazi asiyetetereka na ambaye kazi na juhudi zake hapana asiyejua... “aliendelea *boss* (uk.27).”

v) Kuonyesha mada katika barua au kumbukumbu za mkutano kwa mfano KUH: Ombi Lako la Kujiuzulu.

vi) Kunukuu ukurasa wa Bibilia kwa mfano kasisi alisoma Luka 2:1- 6. Kufuatia matumizi ya kiakifishi hiki kwenye mifano tuliyoirejelea, inabainika wazi kuwa mwandishi alikitumia na lengo la kutoa ufafanuzi zaidi ili msomaji aweze kuelewa ujumbe ambao alilenga kuuwasilisha. Katika kufanya hivyo, mwandishi aliweza kuimarisha uchimuza katika riwaya.

3.3.2.3 Semi koloni (;)

Ezugu (2001) anasema kuwa alama hii hutumika katika uandishi na upigaji chapa. Anasema kuwa hutumika katika matini ili kuleta pumziko kwenye taarifa, ingawa pumziko hilo huwa refu kuliko kipumuo lakini fupi kuliko kikomo. Mifano hii kutoka riwayani ni dhihirisho kuwa kiakifishi hiki kilitumika katika ujenzi wa riwaya teule;

- i) Wanasema ndiyo; eti ‘kimelea’ chako na chao kimoja (uk.13).
- ii) Nukta zikazaa dakika; dakika saa; saa masaa; siku... siku, masiku, miezi na miaka’ miaka na mikaka (uk.15).
- iii) Mapenzi yote ya Mkamandume siku hizi yamemiminiwa ki-Katija; naye kapuuziliwa mbali kama vile hayumo ndani ya dunia ya mumewe. Sasa akabaki anatuta; pumzi juujuu! (uk23).
- iv) Akakumbukia hadithi yake mwenyewe; yake yeye na Time kwa kweli(uk.32).
- v) Ingekuwa yeye ndiye aliyepata mimba isingelikuwa kioja; lakini Viwe! Ama kweli umdhaniaye ndiye kumbe siye (uk.42).

Alama hii pia hutumika kutenganisha virai viwili ambavyo tayari vina vipumuo kwa mfano; “ Ingawa limehodhi katika ardhi pana na kuwanda na kujitana kwa vyumba vyake vine, vyoo vitatu, meko mbili, sebule, mabanda yenye uwanja wa kutosha wa kuanika karafuu; uwanja ambao unaunganisha sehemu nyingine zilizopanuliwa kila mara ukoo ulipokuwa ukipanuka, siku hizi limebaki gofu lenye kutawaliwa na ukimya.

Kando na matumizi haya, alama hii pia hutumika kabla ya kielezi kiunganishi kama vile na, hata hivyo, hata ingawa, kando na miongoni mwa vielezi viunganishi vingine kwa mfano, “Alimsikia yule mpandabaiskeli akimaka huku kwa ustadi mkubwa baadaye, akakwepa pakacha la taka lililotupwa njiani; na katika nukta nyingine, shati lake jeupe lililopeperuka

kwa upepo kama mbwa, lilipotea kwenye kona ya kichocho. Uangalifu kwa jicho la ndani kuhusu matumizi ya kiakifishi hiki unadhihirisha kuwa, kando na kuendeleza mawazo, kiakifishi hiki huleta pumziko kimatumizi.

3.3.2.4 Mabano ()

Ezugu (2001) anasema kuwa alama hii hutumika kutoa maelezo zaidi kuhusu wazo kuu lililomo katika sentensi. Hii ina maana kuwa mabano hayo yanaweza kuondolewa katika sentensi bila kuhitilafiana na maana ya sentensi kimuundo. Anasema kuwa mabano yanaweza kutambulishwa kwa alama za kipumuo au hata deshi kimaandishi. Anasema kuwa mabano ambayo hutambulika kwa matumizi ya alama za mabano zenyewe yanaweza kuondolewa kutoka kwenye sentensi bila kuiathiri sentensi hiyo kimaana; kwa mfano, “mashuzi yasiyokuwa madogo na ambayo harufu yake huhanikiza na kukirihisha chumba kizima na kumfanya Time (anayekuwa macho) kuziba pua” (uk. 90).

Hata siku moja “haijulikani siku gani, maana siku zilikuwa bado hazijavumbuliwa, wala hakukuwa na Alhamisi wala Ijumaa), mwenyezi Mungu aliteremsha Malelejemema kwa shani yake! Pale aliposema, “Na iwe Malelejemema.” Ikawa”(uk.10). “ Ilitokezea siku kama leo (na leo zilikuwa nyingi siku hizi) basi tu usingizi ulikataa kuja na Time akabaki kusumbuka kwa kila jambo: fikra pomoni, wasiwasi wa nyuma na mbele, na hasa mbele anakwenda lakini asikojua” (uk.92). Kwa hakika, kiakifishi hiki kilitumika kutoa maelezo zaidi kwa msomaji, na hivyo basi kuimarisha uchimuzi.

3.3.2.5 Deshi (—)

Chukwu (keshatajwa) anasema kiakifishi hiki pia kinaitwa kistari kirefu na anaelezea kuwa kinavyo matumizi kadhaa. Kwanza inatumika kuonyesha kuwa mzungumzaji amebadilisha mawazo kuhusu aliyokuwa akiyasema. Mabadiliko haya ya ghafla huathiri maana na muundo wa sentensi. Pia inatumika kuonyesha mrejeosawa katika usemi kwa mfano; “Likawa limefunga mbele, nyuma, kulia na kushoto limefunga kote “ (uk. 6).

Matumizi mengine ya deshi ni kwamba inatumika kuonyesha kuwa mzungumzaji anasitasita katika mazungumzo yake, au amepigwa chenga na msamiati mwafaka ambao alinua kuutumia kwa mawasiliano yake, kwa mfano; ‘Sana yamebadilisha maumbo na rangi tu baina ya mawazo na mwisho.’” (uk.1). Hata hivyo, deshi katika muktadha wa riwaya teule imetumika kuzua hisia za ucheshi kwa vile kule kusitasita kunaifanya kazi ya fasihi kuwa na uhai fulani katika utanzu.

3.3.2.6 Udondoshaji (...)

Dhana ya udondoshaji inaweza kutazamiwa kuwilikuwili. Kisarufi, hutambulika kwa matumizi ya alama za nukta tatu kwa mfululizo. Kifasihi, hiki kiakifishi kimepewa mitazamo miwili kwa mujibu bwa Wamitila (keshatajwa). Anaelezea kuwa udondoshaji ni wa aina mbili. Wa kwanza ni ule anaouita udondoshaji mwanzo ambao hutumika kuelezea hali ya

kudondoa herufi za mwanzo za maneno katika kirai au sentensi kwa mfano, ‘mefurahi, ‘meukubali, ‘mezuka. Udondoshi mwingine ni udondoshi mwisho ambao hutumika kama adhidadi ya udondoshaji mwanzo.

Hapa, sauti au herufi zinazodondoshwa huwa kwenye sehemu ya mwisho ya neno au maneno. Alama hii imetumika pakubwa katika ujenzi wa riwaya teule na ilishughulikiwa katika muktadha wa kiisimu. Waldhorn na Zeiger (weshatajwa) wanasema kuwa udondoshaji hutambulika kwa vikomo kadhaa mfululizo kimandishi, na kwamba alama hizi zinapotumika katika mandishi, zinadhihirisha kuwa kuna maneno ambayo yamewachwa nje, ambayo mwandishi anamtaka msomaji ajijazia mwenyewe.

Hata hivyo, Waldhorn na Zeiger (weshatajwa) wanaendelea kujadili matumizi mengine ya alama hizi. Wanasema kuwa inatumika kuepuka marudio katika maelezo kwa mfano, hadi siku ya lahaua..., jambo hili mi’ n’na hakika...; uliyoyasema... hatutayatekeleza (uk. Iii). Pia inatumika kudhihirisha kuwa wazo fulani halikukamilika kwa mfano, nataka kuwajuza...lakini tutekeleze majukumu yetu kama walimu. Alama hii ilitumika riwayani na matumizi yake yaliendeleza uchumi katika riwaya.

3.3.3 Viakifishi tamati au vya nje

Kulingana na Chukwu (2010), hili kundi la viakifishi vya nje hujumulisha kikomo, kiulizi pamoja na alama hisi. Kwa hakika, viakifishi hivi vimetumika kwa ujumla katika ujenzi wa riwaya hii.

3.3.3.1 Kikomo (.)

Chukwu (2010) anasema kuwa alama hii pia hujulikana kama kituo kikuu. Kwa mujibu wake, alama hii huwa na matumizi mengi kiisimu, na miongoni mwa matumizi anayoyaaanisha ni pamoja na;

- a) Alama ya kikomo huwekwa mwishoni mwa taarifa au sentensi kuashiria kuwa taarifa hiyo imefika tamati, kwa mfano;
 - i) Mkamandume alianza kuhisi upepo ukimvaa na kumparamia, yeye na mparapata wake (uk.3).
 - ii) Mkamandume na mparapata wake walionekana ndio pekee *walioichanja mvua* (uk.8).
 - iii) Wakapigana na maporomoko ya maji (uk.8).
 - iv) Mkamandume alipomkaribia huyo mwanamke, hakuweza kumtazama machoni.
- b) Alama hii hutumika kuendeleza dhana ya ufupishaji katika maandishi, kwa mfano, badala ya kusema Profesa Mohamed, S. A. ndiye mwandishi wa riwaya ya *Mkamandume*, tunasema Prof. Mohamed, S. A. ndiye mwandishi wa riwaya ya *Mkamandume*.

Hata hivyo, Chukwu (2010) anasema kuwa kikomo hicho huweza kupuuzwa wakati maneno yaliyofupishwa hujumulisha herufi za mwanzo mwanzo mwa kila neno linalofupishwa ili kuibuka na akronimu ya maneno hayo. Kutokana na mawazo hayo,

akronimu TUKI inatokana na Taasisi ya Uchunguzi ya Kiswahili, CHAKITA Chama cha Kiswahili cha Taifa miongoni mwa akronimu zingine.

Kwa hakika, kiakifishi hiki kimeitawala riwaya hii na kando na matumizi yake kiisimu, alama hii imetumika kudhihirisha kukamilika kwa mawazo katika kifungu ambacho kimebeba habari zilizo kamili. Msomaji wa matini hii kwa hivyo huongozwa na kiakifishi hiki katika usomaji wake ambapo hutambua kukamilika kwa mawazo ya mwandishi kinapotumika. Ifanyikapo hivyo, kiakifishi hiki huwa kimeimarisha uchimuzi wa matini hiyo.

3.3.3.2 Kiulizi (?)

Akishughulikia viulizi, Chukwu (2010) anatueleza kuwa ni vya aina mbili. Anakielezea kiulizi cha kwanza kama kile ambacho kina mzizi {-ni}, ambacho hujumulisha (ni - ni), (na - ni) na (li - ni), ilihali kile cha pili ni kiulizi ambacho hupewa jibu la ndiyo au la. Kiulizi hiki cha pili hujitokeza katika muktadha wa kitenzi. Hata hivyo, anasema kuwa la muhimu ni kuwepo kwa alama ya kiulizi mwishoni mwa kifungu au sentensi hiyo. Anaendelea kusema kuwa alama hii huwa na matumizi yafuatayo:

- a) Kuulizia swali, ikiwa kiakifishi hiki kitapachikwa mwishoni mwa kifungu, kwa mfano
‘‘Sasa madamu ukweli umeshauona na kuujuu Mkamandume, unangojea nini? Kataa. ‘‘

b) Alama hii hutumika kuendeleza upekee. Kulingana na maelezo haya, alama ya kiulizi haitumiki katika maswali yasiyo dhahiri kwa mfano ; Nani asiyejua Mkamandume wa zamani? (Swali dhahiri). Mkamandume alijiuliza ikiwa kulikuwepo na yeyote ambaye hakufahamu alivyokuwa zamani (swali lisilo dhahiri). Mifano hii ni miongoni mwa mingine mingi ambamo kiakifishi hiki kimetumika katika ujenzi wa riwaya. Hata hivyo, inajitokeza wazi kuwa katika muktadha wa kuzungumza na nafsi yake, Mkamandume amejaribu kuleta uhai riwayani kupitia kwa alama hii. Uhai huo, humpa msomaji ufasiri tofauti na katika kufanya hivyo, kazi hiyo inachimuzwa.

3.3.3.3 Alama ya kihisishi (!)

Kulingana na Chukwu (2010), alama hii hupachikwa mwishoni mwa kifungu kudhihirisha hisia nzito. Kulingana naye, katika hali ya kawaida ni nadra kwa watu kuonekana wakitoa hisia nzito. Mtu anapokuwa katika hali ya hatari, ataonekana akidhihirisha hisia zake. Waldhorn na Zeiger (weshatajwa) wanapendekeza kuwa alama hii ni vyema itumike kimaksudi bali siyo katika hali ya kimzaha. Wanasema kuwa, alama hii pia yaweza kutumika kuigizia tanakali za sauti. Tunakumbana na alama hii katika sehemu ya tabaruku, ambako mwandishi anaonyesha hisia nzito kuhusu maisha ya wananchi wa Malelejimena (uk.iii).

Mifano mingi imo katika riwaya kuashiria matumizi ya kiakifishi hiki k.m “wakati huu Mkamandume aliingia kiamboni pake. Rovurovu - kaenea tope kila pahala! Kata, kata, chinja, chinja! Alijikuta kama Fumo Liongo akihujumu maadui zake nguvu mmoja, kasi moja,” pumzi moja” (uk.23). Mifano hii ambamo kiakifishi hiki cha kihisishi kimetumika riwayani ni dhihirisho kamba usimulizi wenyewe umejaa hisia nzito ambazo zinayatishia maisha ya wanajamii.

Uamuzi wa Mtemi wa kutomtuzia mkulima bora katika jamii, ambaye ni Mkamandume unamjaza mhusika huyu hisia nzito za hasira, inayomfanya aifyeke mimea yake ya mihogo na ndizi kwa vile amekata tamaa. Hili ni jambo la kawaida kwa yeyote aliye na hisi. Hata hivyo, kimuktadha, kiakifishi hiki kimetumika kuipa riwaya uhai, bila kusahau kuwa, kinachomtofautisha binadamu na wanyama wengine ni ule uwezo wake wa kuhisi. Kiakifishi hiki kimetumika kuimarisha uchimuzi katika riwaya.

3.4 Viakifishi kimuundo

Watalaamu Waldhorn na Zeiger (1980) na Chukwu (2010) pia wameweza kuviangazia viakifishi kimuundo na kuibuka na mawazo muhimu. Chukwu (keshatajwa) ameshughulikia viakifishi kimuundo katika muktadha wa kisasa. Kwa ufupi tu, ameuzingatia ule muainisho wa vipengele hivyo wa awali na anatueleza kuwa vile viakifishi vya nje au tamati ambavyo

hujumulisha kikomo (.), kiulizi (?) na kihisishi (!) hutumika kimuundo kuelezea kuwa wazo limewasilishwa kwa ukamilifu.

Kulingana na Yeibo (2014), viakifishi kama mojawapo ya vipengele vya kigrafolojia kimuundo hutumika na dhima ya kuwezesha kufululiza kwa mawazo katika matini. Kando na hayo, anasema kuwa alama hizi huchimuza matini kwa ujumla. Anasema kuwa kikomo kinapotumika katika matini, hudhihirisha kuwa ujumbe katika taarifa hiyo umefika mwisho au umekamilika kimuundo. Kulingana naye, alama ya kiulizi hutumika katika matini kumaanisha kuwa kuna ujumbe ambao unahitajika, unaochochewa na kiambishi – ni (**ni - ni**),(**li-ni**), (**na-ni**).

Kwa mujibu wa Yeibo (2010), alama ya kihisishi kimuundo huashiria au hudhihirisha kuakisiwa kwa hisia kuhusu tukio au matukio fulani. Hisia hizi huibua maana fulani ambayo huwasilishwa kupitia kiakifishi hicho. Akichangia, Thurman anayerejelewa katika Chukwu (2010) anasema kuwa iwapo wasomaji na wandishi hawatazingatia mfumo mmoja na msimbo wa matumizi ya viakifishi, matokeo yatakuwa ya kutatiza na kupotosha. Anaendelea kusema kuwa matumizi ya mfumo mmoja humwezesha mwandishi na msomaji kuelewa kinachowasilishwa katika matini. Anasema kuwa kuelewa kinachowasilishwa na mwandishi huendeleza mfululizo wa usomaji na hivyo basi uelewa ambao zao lake ni kufaulisha dhima ya ujumbe uliolengwa na matini hiyo.

Crystal (1995) anasema kuwa viakifishi hubeba maana nyingi katika matini na anatoa mfano wa kikomo ambacho hutumika kimuundo kukamilisha sentensi kimaandishi. Katika riwaya ya *Mkamandume*, mwandishi ametumia alama hii ya kiakifishi kiufundi kuibua mapumziko katika kazi yake. Alama hii inapotumika kiisimu kama pumziko, kasi ya kusoma matini hufifia. Akichangia kuhusu matumizi ya koma kimuundo, anasema kuwa alama hii hutumika kuendeleza pumziko fupi.

Mwandishi wa riwaya hii ametumia alama hizi kimuundo ili kumwezesha mhusika Mkamandume kupumzika huku ujumbe wake ukiwasilishwa, miongoni mwa vitu vinavyotajwa riwayani. Kulingana na wataalam hawa, alama hizi ni muhimu kwa vile zinafanya mandishi kuwa na maana kwa sababu humwezesha msomaji kuweza kupumzika na kufikiria kuhusu ni kipi anachokisoma.

Kulingana na Waldhorn na Zeiger (weshatajwa), uamuzi wa kutumia alama hizi ni dhihirisho la mwandishi mwema. Kando na hayo, wanatoa tahadhari kuwa matumizi ya alama hizi kupita kiasi huharibu kazi ya uandishi.

3.5 Kiishilio

Sura hii ilitupa msingi dhahiri kuhusu dhana ya viakifishi. Aidha, uainisho huo wa viakifishi kwa makundi matatu ulikuwa na manufaa makubwa kwa utafiti huu. Pia mtafiti aliweza kurejelea matumizi ya aina hiyo mbalimbali ya viakifishi katika ujenzi wa riwaya teule, huku

akidondoa mifano mbalimbali. Mchango wa wataalamu mbalimbali kuhusu vipengele hivi vya uakifishaji ulituwezesha kuielewa dhana hii kiundani na dhima yake kimtindo na kimuundo.

SURA YA NNE

VIPENGELE VINGINE VYA KIGRAFOLOJIA VISIVYOKUWA VIAKIFISHI

4 Utangulizi

Sura hii ililenga kuchanganua vipengele vingine vya kigrafojia kando na viakifishi na kuonyesha jinsi vilivyotumika katika ujenzi wa riwaya teule. Aidha, athari yavyo ilichunguzwa kiundani. Kwa mujibu wa Chukwu (2010), kuna vipengele vingine vya kigrafojia ambavyo ni vya kimsingi katika uandishi ambavyo si viakifishi. Miongoni mwa vipengele hivi ni pamoja na maandishi ya *milazo*, herufi kubwa, herufi nzito, na aina mbalimbali za fonti ambazo matumizi yake pia huchangia katika uimarishaji wa uchimuzi.

4.1 Maandishi ya mlazo

Waldhorn na Zeiger (weshatajwa) wanasema kuwa matumizi ya alama za mlazo huweka uzito katika neno hilo, na matumizi yake hujitokeza wazi wakati makala yanapopigwa chapa. Okunoye na mwenzake (weshatajwa) wanasema kuwa matumizi ya maandishi ya mlazo katika matini huwa na umuhimu huu kwa ujumla:

- i. Kurejelea maneno ambayo ni ya lugha tofauti na usimulizi (ya kigeni) katika matini, kwa mfano, alikuwa kavaa *bulbul* (uk.25), ...aliendelea *boss* (uk.27),... *Audhu bin-llah* (uk80) *inafu, batra, La ley delgallinero, Mdi Msumu, huru l-eyn, tiktak* (uk.49), *swin swin, regulator, u-regulator* (uk.49).

- ii. Pia hutumika kusesitiza, kwa mfano katika (uk.26), kulingana na maandalizi ya kutuzwa kwa mkulima bora ambako Mkamandume alikuwa na matarajio makubwa, mhusika huyu anazama sana katika matarajio yake kiasi kwamba, mara kwa mara anajiuliza ;*Zawadi nono itakwenda kwa nani? wapi?*
- iii. Alama hii inatumika kutaja majina ya meli, ndege kama vile Titanic, Boeing 707.
- iv Kuendeleza majina ya majarida, matini ya magazeti, tamthilia, riwaya kwa mfano, *Mkamandume*.
- iv. Kuonyesha nyimbo na mashairi katika riwaya kama vile katika ushairi

uliomo kwenye tabaruku ya riwaya teule ya *Mkamandume* (uk. iii)

‘ N’najua ‘walalaji’ wamelala,

hadi siku ya lahaula.....

Wamalala usingizi ul’ochacha,

kungojea linikutakucha!

Naam, kutakuja kupambazuka,

Jambo hili mi’n’na hakika....

Mungu niweke siku ikifika,

nije kuona mikiki na mikaka!

Mahir kijana wetu

Ushangirie vukutu letu

Vukutu ushindi wetu

Kukata miti na misitu !'

vi. Kunukuu usemi halisi, wito katika matini.

vi Kurejelea msamiati usio wa kawaida kama vile *maamuru* (uk.1), *kweche-*

kweche (uk.2), *aliachia frii*(uk.12), *pechi* (uk.13), *kinuskoti* (uk.26)

Kinachomchafyauk.21), miongoni mwa maneno mengine mengi ambayo

mwandishi aliyatumia.

Mwandishi wa riwaya ya *Mkamandume* ametumia milazo kwa mapana katika ujenzi wa kazi yake. Cha ajabu ni kwamba, kama alivyonena Wamitila (keshatajwa), kuna baadhi ya maneno ambayo mwandishi aliyaendeleza kwa milazo huku akiwa amekaidi othografia ya maneno hayo. Kwa hakika matumizi ya alama hii katika muktadha huu riwayani ulilenga kuukuza na kuupanua msamiati wa lugha ya Kiswahili kando na kuweka uzito kwa

viambajengo hivyo vya lugha. Katika jitihada za mwandishi kutumia alama hizi, ni dhahiri kwamba alilenga kushika makini ya msomaji wa riwaya ili amakinike zaidi katika usomaji wake na kwa kufanya hivyo, aliweza kuimarisha uchimuzi wa kazi yake.

4.2 Herufi kubwa

Hata ingawa alama hii si miongoni mwa zile zilizoshughulikiwa na Chukwu (2010), alama hii hutumika katika uchapaji. Kwa mujibu wa Massamba (2004), alama hii huwa na matumizi mengi ambayo ni pamoja na;

- i) Kuanzisha sentensi kwa mfano, Mkamandume alitunga hamu ya kutaka angalau amwone Silima ikiwa si kumsikia maoni yake yakoje.
- ii) Hutumika kudhihirish kuwa neno linaloanza kwa herufi hiyo ni nomino ya pekee kwa mfano, Mkamandume alianza kuhisi upepo ukimvaa na kumparamia.
- iii) Hutumika kuonyesha kichwa cha mada kwa mfano *Mkamandume*.

4.3 Herufi nzito

Mwandishi wa riwaya ya *Mkamandume* aliweza kuzitumia herufi nzito katika kazi yake. Herufi nzito kwa mujibu wa Chukwu (keshatajwa) huhusu matumizi ya wino mzito katika maandishi. Herufi hizo ziliweza kutumika mwanzoni mwa neno la kwanza katika kila sura kwenye riwaya nzima. Anasema kuwa matumizi ya herufi zenye wino uzito katika neno au uandishi hulenga kuweka msisitizo katika neno hilo. Kwa kufanya hivyo, inadhihirika wazi

kuwa mwandishi alilenga kushika makini ya msomaji katika ufunuzi wa kila sura, ili msomaji aone mfululizo na mvunjiko wa mawazo ya mwandishi katika kila sura.

Neno la kwanza katika sura ya kwanza riwayani ni **Mwanzo**, linaloanza kwa herufi nzito na kubwa **M**. Katika sura ya pili, neno **Sikiliza vile vile** limefuata utaratibu ule ule kama wa sura ya kwanza, na hata ya tatu **Baba**, utaratibu uliyozingatiwa katika sura zote riwayani. Kwa hivyo, kando na kuchimuza maneno hayo, mwandishi anamwelekeza msomaji kuwa na uwezo wa kutambua mfululizo na mvunjiko wa ujumbe wa mtunzi.

4.4 Fonti za maneno

Kipengele kingine cha kigrafolojia ambacho kilijitokeza katika riwaya ya *Mkamandume* ni matumizi ya fonti. Hassan na Elham (2012) walitafiti kuhusu uhusiano uliopo baina ya aina za fonti, kiwango cha ukubwa, nafasi inayowachwa baina ya maneno na kusomeka kwa matini. Katika matokeo yao, inabainika wazi kuwa fonti ya pointi kumi na mbili inasomeka vyema. Rossum akirejelewa katika Hassan anasema kuwa aina ya fonti ambayo mwandishi ataamua kuitumia itachangia pakubwa katika usomaji na upokezi wema wa ujumbe katika matini.

Jaret (2016) anasema kuwa ipo haja kubwa ya kufanya uchunguzi kuhusu athari ya fonti na uwezo wa msomaji kusoma idadi fulani ya maneno kwa dakika moja, kwa vile kasi ya usomaji huathiri ukopezi wa ujumbe. Hata hivyo, hawa wataalam wanakubaliana kuwa matumizi ya fonti kubwa au ndogo huathiri upokezi wa ujumbe kwa msomaji. Adrienne (2016) anasema kuwa fonti aina ya *Times New Roman*, pointi kumi na mbili ndiyo mwafaka katika tafiti za kiakademia. Mwandishi wa riwaya ya *Mkamandume* alitumia fonti aina ya *Times New Roman* pointi kumi na mbili na kufuatia matumizi ya fonti hii, riwaya teule iliweza kusomeka kwa urahisi.

4. 5 Kiishilio

Kutokana na matumizi mengine ya alama za kigrafolojia zisizo viakifishi katika riwaya ya *Mkamandume*, imetambulika wazi kuwa alama za mlazo, herufi kubwa, herufi nzitona fonti mbalimbali zina mchango mkubwa katika ujenzi wa riwaya teule, na kwamba vinaathiri upokezi wa ujumbe uliolengwa na mwandishi, na kwa kufanya hivyo, huimarisha uchimuzi wa matini.

SURA YA TANO

UFUPISHO WA MATOKEO YA UTAFTI, HITIMISHO PAMOJA NA

MAPENDEKEZO.

5. Utangulizi

Katika sura zilizotangulia, tulichanganua dhana ya grafolojia na uchimuzi katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa kimtindo na kimuundo, huku tukilenga jinsi vipengele vya kigrafolojia; hususan viakifishi vilivyotumika katika ujenzi wa riwaya ya *Mkamandume*. Sura hii inatoa muhtasari wa kazi nzima iliyotafitiwa, huku matokeo ya utafiti, changamoto zilizojiri, pamoja na mapendekezo yakiainishwa waziwazi.

5.1 Muhtasari wa utafiti

Utafiti huu ulilenga kutathmini ikiwa vipengele vya kigrafolojia vilichangia katika ujenzi wa riwaya teule ya *Mkamandume*. Baada ya tathmini hiyo, utafiti ulibainisha ni vipengele vipi vya kigrafolojia vilivyotumi na kuchanganua athari ya matumizi ya vipengele hivyo kwa msomaji. Ni utafiti uliyoendelezwa kwa utaratibu uliyojikta katika sura mbalimbali zilifuatazo:

Sura ya kwanza ilizingatia vipengele muhimu vya kimsingi katika utafiti. Hivi vilijumulisha usuli wa mada ulivyobainisha jinsi mada hiyo ilivyoibuka, suala la utafiti, malengo, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka na msingi wa nadharia iliyoungozwa utafiti huu. Iliweza kubainika kwamba dhana ya grafolojia ni pana na haijashughulikiwa kwa

undani katika utanzu wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa kama ilivyoshughulikwa katika utanzu wa Ushairi katika Kiswahili.

Sura ya pili ilichanganua riwaya ya kisasa katika miktadha au mazingira ya Kimagharibi na Uswahilini. Katika uchanganuzi wa mtafiti, iliweza kubainika kuwa msingi wa utanzu wa riwaya ya Kimagharibi na Uswahilini unatofautiana kiwakati na kimaudhui na kwamba riwaya ya Kiswahili ya kisasa inaweza kuchangia katika ukombozi wa jamii kwa ujumla kutokana na ukakamavu unaodhihirishwa na waandishi wa riwaya hizi.

Sura ya tatu iliihakiki riwaya ya *Mkamandume* kimuhtasari na kimuktadha, huku vipengele vya kigrafolojia; viakifishi vilivyotumika na mwandishi katika ujenzi wa riwaya ya *Mkamandume* vikijadiliwa. Mtafiti aliweza kubaini kuwa kuna aina tatu ya viakifishi ambavyo alivijadili na kudhihirisha jinsi vinavyotumika katika ujenzi wa riwaya teule na athari kwa msomaji.

Katika sura ya nne vipengele vingine vya kigrafolojia, visivyokuwa viakifishi vilichanganuliwa Aidha, iliweza kubainika kwamba mwandishi wa riwaya ya *Mkamandume* alitumia alama za milazo, herufi kubwa, herufi nzito na fonti aina ya Times New Roman 12 katika ujenzi wa riwaya ya *Mkamandume*. Athari ya matumizi ya alama hizi pia iliweza kubainishwa.

Sura ya tano ilirejela ufupisho wa yaliyotangulia, mafanikio na changamoto pamoja na mapendekezo kwa ajili ya tafiti za baadaye.

5.2 Matokeo ya utafiti

Kutokana na utafiti huu, ilibainika kuwa vipengele vya kigrafolojia ni vingi na vina mchango mkubwa katika ujenzi wa riwaya teule ya *Mkamandume*. Hii ilibainika wazi tuliporejelea riwaya za Kiswahili za awali ambazo zilijumulisha *Kusadikika* (1951), *Simu ya Kifo* (1965), *Kisima cha Giningi* (1968) na *Utubora Mkulima* (1968). Katika mkusanyiko huo wa riwaya, ilidhihirika wazi kuwa matumizi ya vipengele vya kigrafolojia ilikithiri. Hata hivyo, iliweza kubainika kwamba vipengele vya kigrafolojia vilitumika wakati huo na lengo la kukuza msamiati wa Kiswahili kwa vile matumizi ya lugha ya Kiswahili yalikuwa hayajaenea sana kama ilivyo leo.

Utafiti huu uliweza kuonyesha kwamba riwaya ya kisasa ya Kiswahili imepiga hatua kubwa katika uandishi wake kama inavyodhihirika kwa matumizi ya vipengele vingi vya kiisimu; vya kigrafolojia kando na maneno yaliyotumika. Iliweza kubainika kuwa kuna mchango kubwa wa matumizi ya aina mbalimbali ya viakifishi katika ujenzi wa riwaya teule, huku vipengele vingine visivyo viakifishi ambavyo ni milazo, herufi kubwa, fonti na herufi nzito vikiangaziwa.

Vipengele hivi viliweza kuchanganuliwa kimtindo na kimuundo, na athari zake kwa msomaji ziliweza kutambulika waziwazi, huku athari kuu ikiwa uimarishaji wa uchimuzi. Kando na

kuimarisha uchimuzi, vipenegele hivi vilichangia pakubwa katika kuwasilisha ujumbe kwenye matini na kukuza msamiati wa Kiswahili.

Kando na matokeo hayo, ilibainika wazi kuwa vipengele hivi vilitekeleza jukumu la kiuajumi au kuongezea madaha katika riwaya, kwa mfano matumizi ya ving'ong'o. Iliweza kubainika kwamba ingawa vipengele hivi havijapewa uzito kwa kutafitiwa na kuhusishwa katika uhakiki wa riwaya, mwandishi wa riwaya anayevipuuuzilia mbali katika uandishi na uhakiki wa kazi yake ni sawa na mwandishi asiyejua analolifanya. Hii ilitokana nilipotambua kwamba vipengele hivi ndivyo hutambulika mwanzoni mwa matini, kwa vile hutambuliwa kwa macho, na kwamba, hubeba ujumbe fulani wa kipragmatiki ambao huathiri ufasiri katika usonde.

5.3 Changamoto katika utafiti

Changamoto kadhaa zilidhihirika wakati wa kutafitia kazi hii. Changamoto ya kwanza ilihusu dhana ya riwaya ya kisasa na riwaya ya Kiswahili ya kisasa. Ilikuwa vigumu kuchora mipaka, mahala ambapo riwaya ya awali ya Kiswahili inapofikia, na pale ambapo riwaya ya kisasa ya Kiswahili huanzia, kutokana na mitazamo mbalimbali ya wananadharia wa riwaya ya kisasa.

Changamoto ya pili ilihusu tafsiri na ufasiri wa mawazo mbalimbali ya wananadharia wa kimtindo na wataalam wengine kuhusu mchango wa isimu katika utanzu wa riwaya. Hii

iliweza kuzua changamoto kwa vile michango yao mingi iliweza kuwasilishwa kwa lugha ya Kiingereza, na harakati za kutafsiri na kufasiri huzua utata.

Kando na changamoto hizo nilizozitaja, naweza kusema kuwa kwa muda mrefu nilikuwa yatima katika shughuli hizi za utafiti. Hii ilitokea baada ya kuachwa na msimamizi wangu mmoja wa awali, baada ya uamuzi wake wa kujitosa katika siasa bila kuniarifu au kunijulisha. Hii iliuathiri utafiti huu kwa kuufanya uchukue muda mrefu.

5.4 Mapendekezo kwa ajili za tafiti za baadaye

Utafiti huu ulichunguza viakifishi kama mojawapo ya vipengele vya kigrafolojia vilivyotumika katika ujenzi wa riwaya ya kisasa. Hata hivyo, nivyema ikiwa utafiti mwingine utafanywa kuhusu mchango wa vipengelevingine vya kigrafolojia kama vile ukiukaji wa othografia ya maneno, mchango wa katuni katika kuimarisha mawasiliano na hata athari za kilahaja za mwandishi katika ujenzi wa riwaya za kisasa za Kiswahili na jinsi zinavyoweza kumuathiti msomaji. Ni vyema ikiwa wahakiki wa riwaya za Kiswahili watazingatia mchango wa vipengele hivi ya kiisimu , kando na maneno katika uhakiki wao.

MAREJELEO

Abedi, K. A. (1954) *Sheria za Kutunga Mashiri*. Nairobi: E. A. L. B

Abdulla, M. S. (1968). *Kisima cha Giningi*. Nairobi: Evans Brothers Ltd.

Adegoju, A. (2008) ‘*Graphology as a signifying system*’ katika taarifa rasmi ya habari

ya chuo Kikuu cha Ibadan katika makala ya Atoye, R. O.(Ed). Papers in

English and Linguistics, juzuu ya 9.

Adrienne, W. (2016). *The Psychology of Fonts & Their Impact on Conversions*.

Undullify.com.

Alo, M. (1998). *Style in Language and Communication*. Port Harcourt: Aeddy Link.

Bal, M. (1985). *Narratology: Introduction to The Theory of Narrative*. Toronto:

University of Toronto Press.

Barth, J. (1984). *The Literature of Replenishment*. London: John Hopkins University

Press.

Bleiman, B., Ogborn, J. & Webster, L. (2001). *The Modern Novel Critical*

Approaches. London: The English & Media Centre.

Bradford, R. (1997). *Stylistics*. London: Clays Ltd.

Buffons, G. (1930). *Buffon's Discourse on Style*. Paris Librarie: Haitier Publishers.

Chukwu, E. (2010). *Graphological Elegance of English Punctuation Notations in the*

Journal of Religion and Human Relations, juzuu 1 namba 3 October 2010.

Crystal, D. & Davy, D. (1969) *Investigating English Style*. London: Longman Ltd

Crystal, D. (1987). *Child Language, Learning and Linguistics*. London: Edward

Arnold Publishers Ltd.

Crystal, D. (1995). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Great Britain:

Cambridge University Press.

Dámová, P. (2007). *A Stylistic Analysis with a Focus on Lexical*

(Binomial) Expressions. Masaryk University in Brno: Faculty of

Education, department of English Language and Literature. English

Language, *Course No. 447b of Rapid Results College (uk.79)*

<http://www.ajol.info/index.php/jrhr/article/download/87346/77061>

Ezugu, M. A. (2001). *Fundamentals of English Language and Literature for*

Tertiary Institutions. Enugu: School of General Studies, MT.

Galperin, I. R. (1981). *English Stylistics*. Moscow: Vyasaja Scola.

Gromov, M. (2014). "Visions of the future in the 'new' Swahili novel" *Hope in*

desperation ? Tydskrif Vir Lettrkunde. Nairobi: U.S.I.U

Hassan, S. & Elham, M. (2012). "The Effect of Text Typographical Features on

Legibility, Comprehension, and Retrieval of EFL Learners." *English*

Language Teaching; juzuu ya. 5, namba 8; 2012 Department of Applied

Linguistics. Tehran: Payame Noor University.

Jaret, S. (2016). *Quantitative Analysis of Font Type's Effect on Reading*

Comprehension. Clemson: Clemson University.

Katalambulla, F. H. H. (1965). *Simu ya Kifo.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kezilahabi, E. (1980). "The Swahili Novel and the Common Man in East Africa,

katika " *The East African Experience.* Ulla Schild (Mh.) Reimer: Berlin.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona.* Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam U.P.

Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile.* Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam U.P.

Khaled, N. (2012). *Stylistics and style: Concepts and Theories.*

shodhganga.inflibnet.ac.in/bitstream/10603/4248/10/10_chapter%205.pdf

Kiiru, M. (2003). *A Case for Stylistics in Literary Scholarship Review of Niyi*

Osundare, Cautious Paths through the Bramble, Ibadan: Hope Publications,
2003. University of Nairobi.

Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha
Tanzania.

Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.

Leech, G. N. & Short, M. H. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to
English Fictional Prose*. New York: Longman Group Limited.

Leech, G. N. & Short, M. H. (2007). *Style in Fiction* (2nd Ed.). London: Pearson
Education Ltd.

Longacre, R. E. (1992). *Language in Context: Essays by The Summer Institute of
Linguistics and the University of Texas at Arlington Inc.* Library of Congress
Katalogi namba: 92-80356.

Marie, L. (2013). "Charaterization Through Stylistic Variation in First- Person
Narratives". Paris: Masters Thesis.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam:
TUKI.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*, Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mehmood, A., Saddique, G. & Summara, R. (2014). "An Analytical Study of E. Cummings' Poem "Buffalo bill's" Pakistan: European Journal of Research and Reflection in Arts and Humanities, juzuu 2 namba 2.

Meyer, M. (1997). *The Compact Bedford Introduction to Literature. Reading. Thinking. Writing.* Boston: Bedford Books St. Martin's Press.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Miall, S. & Kuiken, D. (1995) "Aspects of Literary Response:" *A New Questionnaire*, Toronto: University of Alberta. *National Council of Teachers of English*, juzuu 29, namba 1.

Mlacha, S. A. K. & Madumulla, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dares Salaam University Press.

Mkangi, K. (1978) *Ukiwa*. Nairobi: O.U.P.

Mkangi, K. (1993). *Walenisi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi: E.A.E P.

Mohamed, S. A. (2002). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Longman.

Mohamed, S. A. (2013). *Mkamandume*, Nairobi: Longhorn Publishers.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Muriuki, N. K. (2013). *Mtindo katika Nyimbo za kazi za jamii ya Warabai*.

Nairobi: Kenyatta University.

Namayi, C. (2012). "Metaphors of Power in Selected Kenyan Plays: A Comparative

Study of Inheritance and the Hunter is Back." Nairobi: Tasnifu ya M.A,

Kenyatta University.

Ngara, E. (1982). *Stylistic Criticism and the African Novel*. Nairobi: Heinemann

Educational Books Ltd.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu*.

Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ogunsiji, A. (2007). *Aspects of Phono - Graphological Design in Soyinka's Faction*.

Iliyohidiwa kutoka: [http:// www.nbleworld.biz/images/ Ogunsji.pdf](http://www.nbleworld.biz/images/Ogunsji.pdf).

Ogunsiji, A. E & Dauda, M. O. D. (2013). *Literary Stylistics*. Lagos: National Open

University of Nigeria.

Ohly, R. (1981). *Aggressive Prose. A Case Study in Kiswahili Prose of the Seventies*.

Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Olali, T. (2008). *Mafamba*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Olali, T. (2012). *Watu wa Gehenna*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Okunoye, N. & Odebunmi, A. (2003). “ Different story, different strategy:

A Comparative Study of Achebe’s Style (S) in A Man of the People and

Anthills of The Savannah”. *Studia Anglica Posnaniensia*, 39, 289-301.

Omar A. A. (2014). *Nafasi ya Hadithi Simulizi Katika Kufunza Maadili Mema*

Shule za Sekondari Visiwani Zanzibar. Tasnifu iliyowasilishwa

kwa ajili ya kutimiza sharti pekee la kutunukiwa digri za

uzamifu (Ph.d Kiswahili) ya chuo kikuu Huria cha Tanzania.

Parsons, D. (2007). *Theorists of the Modernist Novel*: New York. Routledge.

Peer, W. V. (1986). *Stylistics and psychology*. London: Croom Helm Ltd.

Robert, S. (1959). *Diwani ya Kusadikika*. Nairobi: Evans Brothers Ltd .

Robert, S. (1968). *Diwani ya Utubora Mkulima*. Nairobi: Evans Brothers Ltd.

Senkoro, F. E. M. K. (1977). *Riwaya ya Kiswahili na Maendeleo ya Umma*. Tasnifu

ya Uzamili chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Shariff, I. N. (1988). *Tungo Zetu. Msingi wa Mashairi na Tungo Nyinginezo*. Trenton:
The Red Sea Press.

Solomon, J. S. & Chuah, A. B. (2009). *Dictionary of Correct English Usage* Oxford:
O.U.P.

Taylor, T. J. (1980). *Linguistic Theory and Structural Stylistics*. Oxford:
Pergamon Press.

Verdonk, P. (2002). *Stylistics*. Oxford: Oxford University Press.

Waldhorn, A. & Zeiger, A. (1980). *English Made Simple*. London: W.H. Allen.

Wamitila, K. (2002). *Bina-Adamu*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus
Publications.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi, Simulizi na Andishi*. Nairobi:
Focus Books, English Press.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi, Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*.
Nairobi: Vide-Muwa, Daisy Printers.

Widdowson, H.G. (1975). *Stylistics and the Teaching of Literature*.

Hongkong: Longman Group Ltd.

Yeibo, E. (2014). “ Graphological Foregrounding in Chimamanda Adichie’s purple

Hibiscus”. *International Journal of Language and Linguistics*.

Zhukovska. V. V. (2010). *English Stylistics: Fundamentals of Theory and Practice*.

www.academia.edu/.../English_stylistics

Yoshifumi, S. (1997). *Style and Creativity: Towards a Theory of Creative Stylistics*.

Ph.d Thesis. University of Nottingham.